



Karibu Marekani

Kitabu cha Mwongozo
kwa Wakimbizi

Swahili

E

M

O

C

L

E

W

CAL

KARIBU

MAREKANI

Kitabu cha Mwongozo kwa Wakimbizi

Toleo la Tatu
2007

Kimetayarishwa na Center for Applied Linguistics
Cultural Orientation Resource Center
Washington, DC

Wawakilishi kutoka mashirika yafuatayo wamechangia katika toleo hili la kwanza la *Karibu Marekani: Kitabu cha Mwongozo kwa Wakimbizi*:

African Services Committee of New York
Center for Applied Linguistics
Church World Service
International Catholic Migration Commission
International Institute of Erie, Pennsylvania
International Organization for Migration
International Rescue Committee
Iowa Department of Human Services
Jewish Family Services of Baltimore
Lutheran Social Services of Fargo, North Dakota
Lutheran Social Services of the National Capitol Area
Maryland Office of Refugee Affairs
Office of Refugee Resettlement
Refugee Services Alliance of Houston
United Catholic Conference of Bishops
World Relief

Pamoja na wawakilishi walioorodheshwa hapo juu, wawakilishi wa mashirika yafuatayo wamechangia katika toleo hili la sasa:

Arlington Refugee Services, Catholic Diocese of Arlington,
Virginia.
Hebrew Immigrant Aid Society
Immigration and Refugee Services of America

Mashirika yafuatayo yamechangia picha:

Arizona International Refugee Consortium, Inc.
Center for Applied Linguistics
Lutheran Social Services of Fargo, North Dakota
Lutheran Social Services of the National Capital Area
PhotoDisc Inc.
SAGART design

Jalada limetengenezwa na Chroma Design

Usanii wa ndani na toleo limetengenezwa na SAGART design

Karibu Marekani: Kitabu cha Mwongozo kwa Wakimbizi kinawapa wakimbizi wanaopatiwa makazi mapya Marekani habari ya ujumla kuhusu mambo gani wayataraji na huduma gani wanaweza kupata mnamo miezi yao ya mwanzo nchini. Lengo la mwongozo huu ni kuwasaidia wakimbizi hawa kuwa na matarajio sahihi kuhusu kuajiriwa, elimu, huduma za afya, na hali nyingine za maisha katika Marekani.

Mwongozo huu umeandikwa chini ya uongozi wa Ofisi Idadi ya Watu, Wakimbizi na Uhamiaji (Bureau of Population, Refugees, na Migration) ya Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje (US Department of State). Maofisa wa serikali ya nchi na ya majimbo, wawakilishi wa mashirika ya makazi mapya, na wakimbizi waliopatiwa makazi mapya hivi karibuni wamechangia yaliyomo katika mwongozo huu.

Mwongozo huu unapatikana kwenye lugha mbali mbali na umesambazwa kwenye vituo vya taratibu za safari vilivyoko nchi za nje na miongoni mwa wakimbizi ambao wameshakubaliwa kuingia Marekani lakini hawajatimiza taratibu zao za safari bado. Mwongozo huu unasambazwa miongoni mwa wale wanaotoa huduma za makazi mapya ili wajue habari wanazopata wateja wao walio wakimbizi kabla ya kufika Marekani.

Karibu Marekani: Kitabu cha Mwongozo kwa Wakimbizi kinachukua nafasi ya toleo la kabla la wakimbizi, Mwongozo wa Kupatiwa Makazi Mapya Marekani.

Mwongozo huu wote unaweza kunakiliwa. Lakini, picha na nukuu haziwezi kuchapishwa au kutumiwa kwa madhumuni nyingine yoyote ile bila ya kupata kibali kutoka kwa mashirika ya wafadhili .

Utangulizi	3
Kabla ya Kufika Marekani	7
Shirika la Makazi Mapya	17
Huduma za Jamii	21
Nyumba	29
Usafiri	37
Kazi	41
Elimu	59
Huduma za Afya	69
Uangaliaji wa Matumizi ya Fedha	77
Haki na Majukumu ya Wakimbizi Marekani	85
Kujirekebisha Kiutamaduni na Kupata Wajibu Mpya	93



Karibu Kwenye Maelezo ya Utamaduni!


Kitabu cha mwongozo *Karibu Marekani* kitakusaidia kujitayarisha katika miezi yako michache ya kwanza nchini Marekani. Kinakueleza juu ya mambo ya kuyataraji wakati wa kutafuta mahali pa kuishi, kutafuta kazi, kukutana na Wamarekani, na kujirekebisha kwenye utamaduni na jamii ya Marekani.

Kupata makazi mapya ni harakati ndefu na ngumu, na mwongozo huu huenda usiweze kujibu maswali yote ambayo utakuwa nayo juu ya hali yako. Kama una maswali ambayo mwongozo huu hauna jibu au kama kuna jambo hulielewi katika kitabu hiki, uliza wafanyakazi katika kituo cha taratibu za safari (JVA au OPE) au shirika lako la makazi mapya. Wanaweza kukusaidia kupata habari unazozihitaji.

Kuhusu Marekani

Marekani ni nchi kubwa yenye hali ya jiografia na hali ya hewa tofauti. Mchanganyiko wa watu na sheria za mahali hutofautiana kutoka jamii moja hadi jamii nyingine, na kila jamii ina njia zake za kushughulikia wageni. Kwa sababu hiyo, habari ulizosikia kuhusu Marekani, hata ikiwa umezisikia kutoka kwa jamaa na marafiki ambao tayari wako Marekani, huenda zikawa si sahihi. Wafanya kazi kwenye shirika lako la makazi mapya watakusaidia kujifunza juu ya jamii yako mpya na kuelewa mambo gani ya kuyataraji.

Kujua Kiingereza kutakuwa muhimu katika mafanikio yako Marekani. Ijapokuwa utaweza kupata kazi hata kama hujui Kiingereza, lakini nafasi za kazi zitakuwa chache. Kujifunza Kiingereza kutakusaidia kupata kazi bora zaidi, kuelewa mambo wanayosoma watoto wako shuleni, na kufanya marafiki kwenye jamii yako mpya.



Kuhusu Wamarekani

Wamarekani wengi wanathamini tabia ya kujitegemea na kuwa na bidii ya kazi. Mategemeo yao ni kuwa wageni watapata kazi haraka iwezekanavyo ili wajiangelie wenyewe pamoja na familia zao. Wanategemea pia kwamba wageni wasiozungumza Kiingereza watajifunza lugha hii haraka iwezekanavyo.

Wamarekani wanaheshimu watu wanaouliza maswali. Wanaamini kwamba kuuliza maswali kunaonyesha kwamba unajaribu kujifunza na kuelewa. Usipojua kufanya kitu fulani, usiopoje kuuliza. Wamarekani wengi watafurahi kukusaidia.

Tangu Septemba 2001, baadhi ya Wamarekani wamekuwa hawaamini watu wasiovaa nguo zisizo sawa na zile za nchi za magharibi au kwa njia fulani wanaonekana kama wageni. Watu wachache huenda wakaonekana wamehamaki au kutuhumu wageni. Lakini Wamarekani wengi watakukaribisha na watataka kujifunza kuhusu utamaduni wako. Ukipata usumbufu wowote, zungumza na wafanyakazi wa shirika lako la makazi mapya. Watakusaidia na watakueleza cha kufanya.

Kuhusu Makazi Mapya

Makazi mapya yatabadilisha maisha yako. Ni hatua ya kwanza ya kuwa mwananchi wa daima na raia wa Marekani. Wakimbizi waliokuja kabla yako wanasema kwamba katika Marekani wageni wana nafasi ya kujenga upya maisha yao. Kuanza maisha mapya si rahisi, lakini inawezekana. Zaidi ya wakimbizi milioni mbili wamekuja kabla yako, na wengi wao wamefanikiwa. Pamoja na vipaji ulivyonavyo, ujuzi wako, na ushujaa wako, wewe pia utafanikiwa.

Tunakutakia kila la kheri.



Sasa, kwa vile ofisi ya Huduma za Uraia na Uhamiaji za Marekani (U.S. Citizenship and Immigration Services (USCIS)) imekupa kibali cha muda cha kuingia Marekani, hatua chache tu zaidi zinatakiwa kabla ya safari yako. Wewe na familia yako lazima mfanye uchunguzi wa kiafya na mfaulu ukaguzi wa usalama. Itabidi wafanyakazi wa kituo cha taratibu za safari wawapelekee habari zako wafanyakazi wa shirika lako la makazi mapya nchini Marekani. Shirika la Kimataifa la Uhamiaji (The International Organization for Migration (OIM)) lazima watayarishe safari yako. Wakati unaposubiri kusafiri unaweza kujifunza kuhusu nchi ya Marekani na kujifunza Kiingereza kama inawezekana.

Uchunguzi wa Kiafya

Uchunguzi wa kiafya unahitajiwa kwa watu wote katika familia yako. Uchunguzi wa kiafya ni bure, na wafanyakazi wa kituo cha taratibu za safari watafanya miadi ya tarehe ya kufanyiwa uchunguzi wa kiafya. Matokeo ya uchunguzi wa kiafya yatatumiwa ifuatavyo:

- yataamua kama wewe au watu wengine katika familia yako mna matatizo ya kiafya na wanahitaji matibabu;
- yatahakikisha kwamba hakuna maradhi ya kuambukiza ambayo yatakufanya wewe au jamaa mwingine katika familia yako asiweze kusafiri Marekani; na,
- yatapeleka katika shirika lako la makazi mapya habari juu ya hali ya kiafya ambayo itahitaji kufuatiliwa utakapofika kwenye jamii yako mpya.

Kwa sasa, matokeo ya uchunguzi wa kiafya yatatumika kwa muda wa mwaka mmoja. Sera hii ya mwaka mmoja inaweza kubadilika katika siku zijazo. Kama hutasafiri katika muda wa mwaka mmoja baada ya kufanya uchunguzi wa kiafya itabidi ufanye uchunguzi wa kiafya mwingine kabla hujaondoka kwenda Marekani. Kwa wale wenye matatizo fulani ya kiafya, kama vile kifua kikuu (TB) au (HIV/ukimwi), matokeo ya uchunguzi wa afya yatatumika kwa muda wa miezi 6 tu.



Ukaguzi wa Usalama

Ni lazima wakimbizi wote wapite ukaguzi wa usalama unaofanywa na maofisa wa serikali ya Marekani kabla ya kusafiri kwenda Marekani. Kwa kawaida, ukaguzi huu hufanywa kabla ya mahojiano yako na USCIS, lakini baadhi ya wakati ukaguzi wa usalama mwingine huhitajika kabla ya kuondoka.

Uthibitaji wa Udhadini na Shirika Lako la Makazi Mapya

Kila mkimbizi anayekubaliwa kuingia Marekani hupewa shirika la makazi mapya, au mfadhili, kabla ya kuondoka. Kituo cha taratibu za safari kitapeleka habari zifuatazo kwenye shirika lako la makazi mapya:

- Jina lako, umri wako, kiwango chako cha elimu, na kazi yako
- Majina, umri, elimu, na kazi za watu katika familia yako na watu gani katika familia watakaofuatana na wewe.
- Asili yako, nchi unayotoka, na dini yako
- Matatizo yoyote ya kiafya ambayo yatahitaji kuangaliwa utakapofika Marekani



- Majina, anuani, na nambari za simu za jamaa au marafiki wowote ambao tayari wanakaa Marekani

Shirika la makazi mapya litatumia habari hizi kukusaidia kuchagua eneo la makazi yako mapya. Kama familia yako ya karibu (baba, mama, ndugu, watoto) tayari wako Marekani, na umewapa wafanyakazi wa kituo cha taratibu za safari nambari ya simu na/au anuani yao, shirika la makazi mapya litajaribu kufanya makazi yako katika mji wanaoishi. Kama umeomba upelekwe karibu na rafiki au jamaa ambaye si mke au mume, mtoto, mzazi, kaka, au dada, shirika la makazi mapya litazingatia kama itawezekana katika eneo hilo kupata huduma unazohitajia na kama itawezekana kupata kazi huko. Kama kuna jamaa wengine ambao si ndugu wanaozingatiwa kupatiwa makazi mapya Marekani, unaweza kuomba makazi mapya katika jamii moja nao, lakini hakuna uthibiti kama jambo hili litatokea.

Kama shirika la makazi mapya halina habari kamili ya sasa ya familia yako na marafiki ambao tayari wako Marekani, unaweza kupata makazi mapya kwenye mji mbali nao. Wape wafanyakazi wa kituo cha taratibu za safari habari za kutosha kama uwezavyo ili shirika la makazi mapya liweze



kuchagua mahali ambapo patakuwa sawa kwako. Kutoa habari hizi hakutaathiri hali yako ya uhamiaji au kuharakisha safari yako. Habari hizo zitaathiri tu wapi Marekani utaweza kupewa makazi yako mapya. Ni kwa manufaa yako kutoa habari hizi.

Shirika lako la makazi mapya litakapoamua wapi utahamia, wafanyakazi wa shirika watawapelekea uamuzi huu na kibali chao cha kukupa makazi mapya wafanyakazi wa kituo cha taratibu za safari. Kabla ya kuondoka, utaambiwa ni sehemu gani utakayoishi Marekani.

Matayarisho ya Safari na Mikopo ya Safari

Shirika la Kimataifa la Uhamiaji (The International Organization for Migration [IOM]) litatayarisha safari yako ya Marekani na litakuarifu tarehe ya kuondoka. Wewe na familia yako mnaweza kupata mkopo wa kugharimia safari yenu. Watu katika familia yako wenye umri zaidi ya miaka kumi na nane kila mmoja anaweza kupata mkopo wake. Kabla ya kusafiri Marekani, utaweka sahihi kwenye karatasi iitwayo *waraka wa kuahidi*, ikiwa ni ahadi yako ya kuulipa mkopo huo. Miezi michache baada ya kufika Marekani, shirika lako la makazi mapya litaanza kukuletea kila mwezi hati ya deni ya kukutaka uanze kulipa sehemu ya pesa unazodaiwa.



Una miaka mitatu ya kulipa deni lote la mkopo. Pesa unazolipa zinakwenda kwenye mfuko wa kuwasaidia wakimbizi wengine kusafiri Marekani. Malipo yako ya mkopo huu ni hatua ya kwanza ya kuanzisha historia nzuri ya mkopo.

Kama kuna mabadiliko yoyote katika familia yako wakati unaposubiri kusafiri, kama vile kuzaliwa mtoto, lazima uiarifu IOM au wafanyakazi wa kituo cha taratibu za safari. Kukosa kufanya hivyo kutachelewesha kuondoka kwenu.

Kabla ya kuondoka, wafanyakazi wa IOM watakupa bahasha yenye nyaraka za kufika. Bahasha hii itakuwa na kadi yako ya I-94 na fomu za forodha, fomu za afya, nakala za X-ray, na nyaraka za makazi mapya. Chukua uangalifu mkubwa usipoteze bahasha hii ya nyaraka utakapokuwa safarini. Usiifungue na wala usiiweke kwenye mzungu wako wa safari. Lazima uwape maafisa wa uhamiaji bahasha hii unapofika Marekani kwenye kiwanja cha ndege cha kwanza.

Mizigo ya Safari

Mashirika ya ndege yanaweka kiwango juu ya ukubwa na uzito wa mabegi, na idadi ya mabegi ambayo kila mtu anaweza kuchukua. Unaweza kuchukua

mkoba mmoja, usiozidi kilo 5 (ratili 10), kwenye ndege pamoja nawe. Kila mtu anaweza pia kuleta mabegi mawili yasiozidi kilo 23 kila begi moja (ratili 50) ili yawekwe kwenye sehemu ya mizigo ya ndege. Hakikisha mabegi yenu na mizigo mingine yamefungika vizuri ili msipoteze chochote safarini.

Hairuhusiwi kuchukua mizigo ya ziada kwenye ndege. Itabidi uisafirishe mizigo ya ziada kabla ya safari na ulipie mwenyewe.

Forodha ya Marekani hairuhusu baadhi ya vitu kuletwa Marekani. Kwa mfano, huwezi kuingiza mimea, matunda, mboga, nyama, au madawa ya kulevya. Unaweza kuleta dawa ulizopewa na daktari wako lakini lazima ziwe kwenye vikopo vyenye maelezo. Huwezi kuchukua vitu kama visu, au mikasi kwenye mizigo wako wa mkononi unaouchukua ndani ya ndege. Kama una maswali juu ya vitu unavyoweza kuingiza Marekani waulize wafanyakazi wa IOM.

Mambo Maalum ya Safari ya Kuzingatia

Safari ya kwenda Marekani ni ndefu, kwa hivyo jitayarisha kwa safari ndefu. Kusafiri kunachokesha kwa watu wazima na ni taabu kwa watoto wadogo. Walishe watoto na waambie waende msalani kabla ya kupanda ndege, na lete nepi za watoto. Jichukulie pakiti za vyakula kwa ajili yako na familia yako.

Ndege inaporuka na inapotua, shinikizo huingia kwenye masikio ya wasafiri. Watu wazima na watoto wanaweza kumeza mate au kupiga miayo kuondosha shinikizo masikioni. Wanyonyeshe watoto wachanga wakati ndege inaporuka na kabla ya kutua. Kumeza kinywaji kama maziwa, maji, au maji ya matunda kutapunguza shinikizo katika masikio yao.

Kama utahitaji kiti cha magrudumu, mikongojo ya kuendea, au msaada maalum mwingine wakati uko safarini, hakikisha umewaeleza wafanyakazi wa IOM. Hali kadhalika, kama unakula dawa uliyoandikiwa na daktari, ichukue pamoja nawe ili uwe nayo utakapohitaji.



Kama unasafiri pamoja na mnyama wa nyumbani, lazima ufuata sheria za forodha za Marekani na kanuni za shirika la ndege juu ya usafirishaji wa wanyama wa nyumbani. Lazima ulipie usafiri wa mnyama huyo mwenyewe. Ni muhimu kuwajulisha wafanyakazi wa IOM kama unasafiri na mnyama, ili shirika la makazi mapya Marekani liweze kutafuta makazi yanayoruhusu wanyama wa nyumbani.

Safari Yako


Kama safari yako itakulazimu upitie viwanja vya ndege vingine kabla ya kufika Marekani, wawakilishi wa IOM watakusaidia. Utakapofika Marekani, wawakilishi wa IOM watakutana nawe kwenye kiwanja cha ndege cha kwanza na kukusaidia katika taratibu za kufika.

Maofisa wa uhamiaji wa Marekani watafungua bahasha yenye nyaraka za kufika na kuangalia nyaraka hizo. Kadi yako ya I-94 itapigwa muhuri na utarejeshewa mwenyewe, utachukuliwa chapa ya vidole vyako, na huenda ukapewa waraka wa kukuruhusu kufanya kazi (Employment Authorization Document [EAD]) yenye picha yako. Kadi yako ya I-94 na waraka wa kazi wa EAD ni nyaraka muhimu kwa sababu zinaonyesha kwamba hali yako ya kuwa mkimbizi Marekani ni ya kisheria. Ziweke nyaraka hizi mahali pa salama. Shirika la

makazi mapya litataka kuziona nyaraka hizi utakapofika kwenye eneo lako la makazi mapya na litafanya nakala za nyaraka. Kama ukiona makosa yoyote kwenye nyaraka hizi, tafadhali wajulishe mara moja maofisa kwenye kiwanja cha ndege cha kwanza utakachofika. Ni rahisi kusahihisha makosa mara tu unapoyagundua kuliko kusubiri mpaka mwisho utakapofika kwenye eneo la makazi yako mapya.

Utakapomaliza taratibu za uhamiaji utachukua mizigo yako na utaendelea kwenda kwenye sehemu ya forodha. Maofisa wa forodha wataangalia fomu yako ya maelezo ya forodha na huenda wakapekua mizigo yako. Vitu vilivyomo kwenye mabegi yako vikipata kibali cha forodha, utakuwa tayari kwenda kwenye sehemu ya mwisho ya safari yako.

Huenda ikabidi ukae kwenye mji wa kiwanja cha ndege cha kwanza ulichofika mpaka siku ya pili kwa sababu ukaguzi huchukua muda mrefu. Kama jambo hili likitokea, IOM litafanya mipango ya chumba katika hoteli (na kukulipia) na pia litafanya mipango ya safari za ndege zitakazokufikisha unakokwenda siku ya pili. Utakapofika kiwanja cha ndege cha mwisho, jamaa, rafiki, au mwakilishi kutoka shirika lako la makazi mapya atakutana nawe kwenye sehemu ya kuchukua mizigo. Kama ikitokea, kwa sababu yoyote, hakuna mtu aliyekuja kukutana nawe, tafadhali wasiliana na polisi wa kiwanja cha ndege mara moja na watakusaidia kufanya mawasiliano na jamaa yako au shirika la makazi mapya.



Katika Marekani, serikali inafanya kazi na mashirika ya makazi mapya kuwapa wakimbizi makazi mapya. Serikali inaweka sheria na miongozo na inatoa fedha za huduma za lazima wanazopata wakimbizi. Mashirika ya makazi mapya yanatoa huduma hizi na inawezekana yakatoa msaada zaidi.

Shirika la makazi mapya linaweza kuwa ni shirika la kidini, shirika binafsi, au shirika la watu wa asili fulani. Ijapokuwa baadhi ya mashirika ya makazi mapya yana uhusiano na vikundi vya kidini, hutarajiwi kushiriki katika shughuli za dini zao. Mashirika ya makazi mapya hayaruhusiwi kuwashawishi wakimbizi kuingia kwenye kikundi cha dini fulani.

Shirika lako la makazi mapya litakuwa na ofisi kwenye mji utakaoishi au karibu na mji huo, na kutakuwa na wafanyakazi watakaokusaidia. Kama una jamaa wanaoishi kwenye eneo hilo, jamaa hao wanaweza kukusaidia katika makazi yako mapya. Jamaa hao wanaitwa “anchor relatives” yaani jamaa unaoweza kuwategemea. Baadhi ya mashirika yana watu wanaojitolea na wanaweza kukusaidia utakapofika.

Kuanza Maisha Mapya

Utakapofika, shirika lako la makazi mapya litakuwa limeshakutayarishia mahali pa kukaa. Mahali hapa panaweza kuwa pa kuishi kwa muda mrefu kama kwenye fleti au panaweza kuwa mahali pa muda mfupi ambapo unaweza kukaa pamoja na familia iliyojitolea kukaa na wewe, au pamoja na jamaa, au katika hoteli. Kama utawekwa kwenye mahali pa kuishi pa muda, shirika litakusaidia kupata mahali pa kudumu haraka iwezekanavyo.

Shirika la makazi mapya litalipia gharama zote za mahitaji ya lazima kwa siku 30 za kwanza baada ya kufika. Baadhi ya mashirika yanalipa gharama hizi moja kwa moja. Baadhi ya mashirika mengine yatakupa wewe au jamaa yako fedha ili ulipie gharama mwenyewe.



Kufanya Makazi Mapya

Shirika la makazi mapya litakupa ushauri mnamo miezi 3 ya kwanza baada ya kufika.

Wafanyakazi wa shirika la makazi mapya, wakisaidiwa na jamaa, marafiki, na watu wanaojitolea, watakusaidia ili uizoe jamii yako mpya. Kwa msaada wao, utafanya mambo haya yafuatayo:

- Kupata makazi ya kudumu
- Kupata nguo na vyombo vya nyumbani
- Kupata habari za uwezekano wa kuunganishwa upya na ndugu wa familia waliobaki nje ya Marekani
- Kupata kadi ya huduma za jamii (Social Security) (inabidi uwe na kadi hii ili uweze kupata kazi)
- Kutafuta kazi
- Kuwaandikisha watoto wako shule
- Kujifunza kuhusu mfumo wa pesa wa Marekani
- Kujifunza vipi kutumia usafiri wa umma
- Kupanga kufanya tathmini ya afya na kupata huduma za afya za lazima
- Kutafuta madarasa ya lugha ya Kiingereza
- Kuanza kujifunza kuhusu mila na sheria za Marekani
- Kujifunza juu ya huduma za jamii zitakazoweza kukusaidia



Utahitaji kutumia huduma zinazotolewa na shirika la makazi mapya kwa vizuri, kwa sababu shirika hilo litatoa huduma hizo mnamo siku 90 za kwanza baada ya kufika kwako. Baada ya siku 90 za kwanza, huduma zitakazopatikana zitategemea mahitaji ya watu binafsi na shirika lako la makazi mapya. Huenda ukaelekezwa kwenye shirika jingine kupata mahitaji maalum.

Shirika la makazi mapya halitolipa madeni yako. Itabidi ufanye kazi kupata pesa uweze kujigharimia.

Wafanyakazi kwenye shirika lako la makazi mapya wataweza kukusaidia vizuri zaidi kama utawasiliana nao kwa vizuri. Waambie juu ya hatua ulizopiga, waeleze kwa uwazi mahitaji yako na wasi wasi wako, na jaribu kujirekebisha na kufuata maoni unayopewa.

Kuhamia Mji Mwingine

Kama ukifikiria kuhamia kwenye jamii nyingine, kumbuka kwamba shirika lako la makazi mapya halina jukumu la kukuhamisha, na shirika la makazi mapya la eneo unalohamia halihitajiwi kukusaidia. Kuamua kuhama ni jukumu lako. Kama utakuwa na swali kuhusu kuhama, zungumza na wafanyakazi wa shirika lako la makazi mapya.



Pamoja na shirika lako la makazi mapya, kuna mashirika mengine ya huduma katika jamii yako. Baadhi ya mashirika haya ni mashirika yaliyo katika mji unaokaa, mashirika ya jimbo, au mashirika ya serikali ya nchi; mengine ni mashirika ya kujitolea, kama yale yenye uhusiano na makanisa, misikiti, na mahekalu. Mashirika haya yote yanaitwa mashirika ya huduma za jamii.

Wakimbizi wanastahiki kupata huduma za jamii kama msaada wa pesa na ushauri juu ya ajira, lakini upatikanaji wa huduma hizi unatofautiana kutoka sehemu moja hadi sehemu nyingine. Shirika lako la makazi mapya litakusaidia kujua huduma gani zinapatikana katika jamii yako, kama wewe unaweza kupata huduma hizo, na pia vipi kupeleka maombi yako.

Mashirika ya huduma za jamii hutoa msaada wa muda wa kukusaidia ili uweze kujitegemea. Mashirika ya huduma za jamii yanahakikisha mahitaji yako yatakuwaje kwa kuangalia pato lako, sehemu unayokaa, umri wako, na vipengele vingine. Hali yako ikiendelea kuwa nzuri, shirika linapunguza huduma unazopata au huacha kabisa kuzitoa. Kama hali yako ikiwa mbaya zaidi, unaweza kuendelea kupata huduma kwa muda zaidi. Ni muhimu kukumbuka kwamba huduma hizi hutolewa kwa muda tu; zinaendelea kutolewa mpaka pale utakapoweza kujitegemea mwenyewe.

Huduma za jamii ni msaada kutoka mashirika binafsi, msaada kutoka serikali, na huduma za umma.



Msaada Kutoka Mashirika Binafsi

Mashirika binafsi yanatoa msaada wa huduma tofauti. Idadi na aina ya huduma hizi hutofautiana kutoka sehemu moja hadi sehemu nyingine, lakini jamii nyingi hutoa huduma zifuatazo:

- Ushauri
- Msaada kwa hali yako ya uhamiaji
- Madarasa ya Kiingereza kama lugha ya pili
- Msaada wa kutafuta ajira (ushauri kuhusu kupata kazi na ushauri juu ya mafunzo ya kazi)
- Huduma za tafsiri

Aina moja ya mashirika binafsi yanayotoa msaada katika jamii nyingi yako chini ya chama cha kusaidiana kinachoitwa “Mutual Assistance Association” au MAA. Haya ni mashirika yaliyoundwa na wakimbizi wa zamani kwa madhumuni ya kusaidia wakimbizi na wahamiaji wapya katika jamii. Mashirika ya MAA yanatoa huduma mbali mbali kama maelezo kuhusu

jamii, tafsiri, msaada wa kupata ajira, usafiri, na madarasa ya lugha ya Kiingereza kwa wakimbizi na wahamiaji.

Taasisi za dini kama makanisa, misikiti, na mahekalu yanaweza yakatoa huduma tofauti. Baadhi ya taasisi hizi huwa na madarasa ya Kiingereza kama lugha ya pili kwa watu wazima au kama shule za jioni (baada ya shule) kwa wanafunzi wa shule, na baadhi hutoa nguo za mitumba na vyombo vya nyumbani. Taasisi nyingine hutayarisha programu za wazee.

Msaada wa Serikali

Mashirika ya serikali ya huduma za jamii hutoa huduma mbali mbali. Mashirika haya husaidia watu wenye mahitaji maalum, kama familia zenye pato dogo, wasio na mahali pa kukaa, na walemavu. Wakimbizi wanaweza kupata programu kadhaa za misaada kutoka serikalini. Kwa kawaida programu hizi hutolewa kwenye ofisi ya serikali ya huduma za jamii, lakini zinaweza kutolewa na mashirika binafsi yanayojitolea yakiwemo mashirika ya makazi mapya.

Programu za serikali zimeweka muda fulani unaobidi kufuatwa na miongozo inayoeleza vipi wakimbizi wanaweza kushiriki kwenye programu hizi. Ili kuweza kushiriki, waombaji lazima wajaze fomu zitakazoonyesha ushahidi wa pato na habari binafsi nyingine. Shirika lako la makazi mapya linaweza kukusaidia kupata maelezo juu ya programu hizi na kujua kama unastahiki kupata msaada na vipi kupeleka maombi yako.

Programu zifuatazo ni programu kuu za serikali zinazosaidia wakimbizi:

Programu za msaada wa fedha. Kwa wale wenye shida kupata kazi, programu mbili zinatoa msaada wa muda wa fedha: Msaada wa muda kwa familia zenye mahitaji (Temporary Assisitance for Needy Families [TANF]), kwa wazazi wenye watoto wanaowategemea, na kuna programu ya msaada wa pesa kwa wakimbizi (Refugee Cash Assistance [RCA]), kwa wakimbizi ambao hawajaoa/hawajaolewa



na wakimbizi waliooa/walioolewa ambao hawana watoto wanaowategemea. Programu hizi zina majina tofauti na hutofautiana kwa njia mbali mbali kutoka jamii moja hadi jamii nyingine. Wanaotaka kushiriki katika programu hizi za fedha lazima waonyeshe kwamba wako katika programu ya mafunzo ya kupata kazi au lazima waonyeshe kwamba wanatafuta kazi. Msaada wa pesa unapatikana kwa miezi michache tu.

Programu za msaada wa kusawazisha (Matching Grant Program). Mashirika mengi ya makazi mapya hutoa programu hii badala ya programu za msaada wa fedha kwa wale wakimbizi wanaotaka kufanya kazi lakini wanahitaji msaada wa fedha kwanza. Wakimbizi wanaojiandikisha na programu hii wanaahidi kupata kazi haraka iwezekanavyo. Kwa kuahidi hivyo wanapata msaada wa fedha na ushauri juu ya kupata kazi, na huduma zitakazowasaidia kupata kazi katika miezi 4 ya kwanza baada ya kufika Marekani.

Stempu za chakula (Food stamps). Hii ni programu ya serikali ya nchi ambayo inatoa msaada wa chakula kwa watu wenye pato la chini walio Marekani. Wakimbizi wanaweza kupeleka maombi ya kupata msaada wa chakula kwenye ofisi ya serikali ya mji wanaokaa. Kiwango cha

msaada wa chakula kinategemea ukubwa wa familia na pato lao. Msaada wa chakula unatolewa kama kadi ya plastiki na kadi hii inaweza kutumiwa kununua chakula. Vitu ambavyo si chakula kama sigireti, ulevi, nepi za watoto, bidhaa za karatasi, na sabuni haviwezekani kununuliwa kwa kutumia kadi hii ya stempu za chakula.

Programu nyingine, Women, Infants, and Children (WIC), ni programu ya serikali ya nchi inayowapa msaada wa chakula ya wanawake, watoto wachanga, na watoto. Programu hii inawapa wanawake waja wazito au wanawake waliojifungua hivi karibuni, watoto wachanga na watoto wasiozidi umri wa miaka 5 chakula cha ziada na elimu ya afya.

Pato la ziada kwa walemavu (Supplemental Security Income, SSI). Hii ni programu ya serikali kuu ya nchi ya msaada wa fedha kwa watu walio vipofu, walemavu, au wenye umri zaidi ya miaka 65. Wakimbizi wa aina hii wanaweza kupeleka maombi yao ofisi ya huduma za jamii (Social Security). Ofisi hii ni ofisi inayotoa kadi za dhamana ya jamii.

Msaada wa kulipia gharama za nishati. Hii ni programu ya serikali kuu ya nchi inayowasaidia watu wenye pato la chini kulipa gharama za nguvu za mitambo mbali mbali kama mitambo ya kupasha joto na viyoyozi yaani mitambo ya kuweka baridi. Wakimbizi wanaweza kuomba msaada wa nishati kwenye ofisi ya serikali ya mji wanaokaa. Programu hii haipatikani kila mahali.

Programu za huduma za utunzaji wa watoto. Baadhi ya jamii zinatoa huduma za kutunza watoto bure au kwa malipo ya chini kwa watu wenye pato dogo. Programu hizi hupata fedha zao kutoka serikali ya nchi na huendeshwa na ofisi au kituo cha serikali ya mji, kama kituo cha kutunza watoto wakati wa mchana. Wazazi wanaohitaji msaada wa utunzaji wa watoto wakati wa mchana ili waweze

kwenda kazini au waweze kutafuta kazi wanastahili kupata aina hiyo ya msaada.

Huduma za Umma

Kila jamii ina huduma za umma zinazoweza kutumiwa na watu wote wa jamii. Kujua kuhusu huduma hizi kutakusaidia kutumia huduma zinazopatikana na kuweza kujirekebisha na maisha ya Marekani. Huduma zifuatazo ni baadhi ya huduma muhimu za umma:

Polisi. Polisi wanahakikisha kwamba sheria zinafuatwa na wanahakikisha pia kuweko usalama wa umma. Vile vile wanaitikia mwito wa hali ya dharura ya kiafya, wanasaidia watu waliopotea, wanafanya kazi kwenye mitaa ya miji ili kuboresha uhusiano wa watu wa mitaa hii. Unaweza kuona polisi wakiwa kazini katika jamii yako, wakiwa kwenye motokaa za polisi au kwa miguu. Inabidi uheshimu cheo cha maofisa wa polisi, lakini usiwaogope. Kama polisi akikuambia usimame lazima usimame. Kukimbia kutaeleweka kama alama ya kuwa umefanya kitu kibaya na kunaweza kusababisha matatizo makubwa zaidi. Usimhonge polisi fedha; kufanya hivyo ni kuvunja sheria na kunaweza kusababisha hukumu kali. Kama huwezi kuwasiliana na polisi, omba msaada wa mkalimani au wasiliana na shirika lako la makazi mapya.

Huduma za hali ya dharura. Jamii zote zina idara za kuzima moto na huduma za magonjwa ya ghafula. Kupata msaada wakati wa hali ya dharura, piga simu 911 na opereta atajibu. Ni lazima uwe tayari kumwambia opereta unachohitaji (“Police”— Polisi, “Fire”— Kuzima Moto au “Ambulance”— Ambulansi kwa hali ya dharura ya kiafya) na pia mwambie mahali ulipo. Kama huwezi kueleza tatizo lako kwa Kiingereza, sema “Help” (Msaada) au “Emergency” (Hali ya hatari) na usiweke simu chini. Kuendelea kukamata simu kutamsaidia opereta kujua mahali ulipo.

Maktaba. Jamii nyingi zina maktaba za umma zenye vitabu, magazeti, na habari kuhusu jamii. Vile vile, maktaba nyingi zina sehemu maalum za watoto na mambo ambayo watoto wanaweza kufanya. Ukipata kadi ya maktaba, unaweza kuazima vitabu kutoka maktabani kwa muda wa wiki chache. Lazima uvirejeshe vitabu hivi kwa wakati, au itabidi ulipe faini kama ukiviweka zaidi ya muda uliopewa.

Bustani za Mapumziko na Burudani. Bustani za mapumziko za sehemu unayokaa zina sehemu za kuwa na pikniki, kucheza, na kufanya michezo ya riadha. Idara ya bustani za mapumziko na burudani za sehemu unayokaa huenda ikadhamini shughuli mbali mbali. Shughuli hizi huwa za bure au za kulipa pesa kidogo za kiingilio, kama vile vikundi vya michezo vya watoto, timu za riadha, na shughuli za wazee. Bustani za jimbo na za taifa hutoa nafasi za kufanya michezo na kufurahia mazingira kama milima, misitu, maziwa, mito, na fukoni. Bustani nyingi zina kanuni zinazohusu aina ya shughuli zinazoruhusiwa. Kiingilio cha baadhi ya bustani hizi ni bure lakini bustani nyingine zina ada ya kiingilio.

Unaweza kupata maelezo kuhusu huduma nyingine za jamii kwenye ukurasa wa Elimu na ukurasa wa Afya.



Unapofika Marekani kwa mara ya kwanza, shirika lako la makazi mapya litakuwa limeshakitayarishia mahali pa kukaa. Mahali hapo patakuwa na fanicha na mahitaji ya lazima. Mwanzoni, huenda ukakaa na jamaa ambao wameshafika Marekani kabla yako, au ukakaa na watu waliojitolea kukaa nawe. Huenda pia ukawekwa kwenye fleti, kwenye hoteli, au kwenye kituo cha kukaribisha watu cha shirika fulani. Kama huna mke au mume, unaweza kuwekwa, kwa muda, pamoja na wakimbizi wengine wasio na wake au waume.

Lazima shirika la makazi mapya lihakikishe kwamba una mahali pa kukaa mwezi wako wa kwanza utakapofika Marekani. Kama una jamaa Marekani huenda wakaombwa wakutayarishie mipango ya mahali pa kukaa.

Kupata Nyumba

Baada ya kufika, wafanyakazi wa shirika la makazi mapya watazungumza nawe juu ya mahali pa kudumu. Kutafuta mahali pa kukaa kunaweza kuchukua muda mrefu kwa sababu ni vigumu kupata mahali pa kukaa pazuri. Utataka kupata mahali ambapo utaweza kulipia kodi, mahali penye usalama, na pako karibu na maduka, usafiri wa umma, kazini kwako, na pia karibu na shule za watoto wako.

Kupata mahali pa kuishi, yafuatayo ni baadhi ya mambo unayoweza kufanya:

- Zungumza na wafanyakazi wa shirika la makazi mapya
- Omba ushauri kutoka kwa jamaa na marafiki zako
- Omba ushauri kutoka kwa wafanyakazi wenzako
- Tafuta matangazo ya kukodi “For Rent” kwenye majengo au karibu na majengo
- Angalia gazeti la kila siku kwenye sehemu ya matangazo



- Soma magazeti maalum yanayoorodhesha fleti na nyumba zinazokodishwa
- Tembelea ofisi za kukodisha fleti kwenye majengo ya fleti
- Tafuta kwenye Mtandao (Internet) matangazo ya fleti ambazo zinakodishwa

Aina za Mahali pa Kukaa

Jamii nyingi za Marekani zina aina tofauti za mahali pa kukaa:

- Majengo ya fleti
- Nyumba
- Nyumba za trela
- Vyumba kwenye nyumba au fleti

Fleti ya kukodi kwa kawaida huwa na sehemu zifuatazo: jiko lenye jiko la kupikia, pahala pa kuoshea vyombo, na friji; chumba cha kuzungumzia na chumba cha kulia; chumba kimoja cha kulalia au zaidi ya kimoja; bafu; na sehemu za kuhifadhi vitu. Aina ya fleti ndogo kabisa inayoitwa “studio” ina chumba kimoja tu chenye bafu lake na sehemu ya kupikia.

Gharama za Nyumba na Usalama

Gharama za nyumba zinatofautiana kutoka jimbo moja hadi jingine, kutoka mji mmoja hadi mwingine, na hata baina ya



jamii katika eneo moja. Popote unapoishi, gharama za nyumba ni gharama kuu katika matumizi yako ya kila mwezi.

Fleti ambazo unaweza kumiliki kulipa zinaweza kupatikana kwenye mitaa ya watu wenye pato la chini, mitaa ambayo ina ujambazi wa hali ya juu kuliko kwenye mitaa mingine. Sehemu yo yote utakayoishi, daima funga mlango wa nyumba yako na jua mitaa gani ya kuiepuka wakati wa usiku. Wajue maofisa wa polisi wa mtaa wako ili uweze kuzungumza nao juu ya juhudi za kuondosha ujambazi katika mtaa wako.

Tegemea kuishi kwenye mtaa ambao una mchanganyiko wa watu wa asili na tamaduni tofauti. Majirani zako huenda watakuwa wanatoka nchi mbali mbali na wenye tamaduni tofauti.



“ Kwa maoni yetu ilikuwa fleti nzuri sana yenye vitu vingi ambavyo hatujawahi kuviona kabla.



... Leo ninajua kwamba watu wanaoishi katika mtaa huu ni maskini sana. Fleti ni ndogo kama uko kwenye sanduku.



Lakini pamoja, mimi na watoto wangu tulisafisha kuta za fleti mpaka zikangara kwenye mwanga wa jua hafifu, na tukafurahia starehe ya nyumba yetu mpya.”

Mikataba na Sheria za Kukodi Nyumba

Ukikodi fleti au nyumba, lazima uweke sahihi kwenye makubaliano ya kupanga au mkataba wa kupanga nyumba. Huu ni waraka wa sheria ambao unamhifadhi anayepanga nyumba (wewe) na mwenye nyumba anayepangisha. Mkataba unakuhifadhi na matendo yasiyo ya haki kutoka kwa mwenye fleti au nyumba.

Mkataba unaeleza kiasi gani inabidi ulipie fleti au nyumba kila mwezi. Kodi ya kupanga inaweza kuwa pamoja na gharama za kulipia nishati kama umeme, mafuta ya kuiweka nyumba katika hali ya joto, maji, na uondoaji wa taka taka. Kabla ya kuweka sahihi kwenye mkataba huo, ni muhimu kumwuliza mwenye nyumba kama gharama za nishati zitakuwemo katika kodi.

Unapoweka sahihi kwenye mkataba, unakubali mambo yafuatayo:

- Idadi ya watu watakaishi kwenye fleti au nyumba
- Jumla ya malipo ya kila mwezi
- Siku maalum katika mwezi ambayo itabidi kodi ilipwe
- Hali ya fleti (itabidi iwe safi bila ya uharibifu wowote)
- Idadi ya miezi ambayo utakaa (kwa kawaida miezi 12)
- Masharti ya kuhamia fleti nyingine kabla ya muda wa mkataba wako kumalizika

Unaweza kutakiwa utoe ushahidi kama utaweza kulipa kodi ya kupanga. Kama hufanyi kazi, basi huna historia ya malipo inayoweza kuonyesha kwamba una historia nzuri ya kulipa madeni yako.

Kwa sababu hiyo, itabidi utafute mtu ambaye ana historia nzuri ya malipo aweke sahihi kwenye mkataba pamoja na wewe.

Kwa kawaida wapangaji wanatakiwa walipe fedha za hifadhi wanapoweka sahihi kwenye mkataba. Fedha hizo za hifadhi kwa kawaida ni sawa na kodi ya mwezi mmoja na utarudishiwa utakapoondoka kwenye fleti kama umetekeleza makubaliano yote ya mkataba.

Kama ukivunja makubaliano ya mkataba unaweza kutolewa kwenye fleti na kupoteza fedha zako za hifadhi. Kwa mfano, majimbo na miji huwa na sheria za nyumba zinazoweka kiasi cha watu ambao wanaweza kuishi kwenye eneo fulani. Hii ina maana kwamba kama una familia kubwa, itabidi ukodi zaidi ya fleti moja. Shirika lako la makazi mapya litajitahidi kukupatia fleti mbili au zaidi zilizo karibu.

Kama una watu wengi wanaoishi kwenye fleti kinyume cha sheria unaweza kutolewa kwenye fleti.

Sheria za kukodi nyumba zinawahusu wenye nyumba na wanaopanga nyumba. Lazima wenye nyumba wahakikishe kwamba fleti au nyumba wanayokodisha zinafuata matarajio ya usalama na hali ya usafi ya mahali panapokodishwa. Mwenye nyumba lazima ahakikishe kwamba umeme, mabomba ya maji, na mitambo ya kupashia moto nyumba vinafuata sheria, na lazima aweke mitambo ya kuhadharisha watu wakati ukitokea moto na ahakikishe kwamba eneo analopangisha halina panya wala wadudu. Sheria za nyumba zinasisitiza kwamba mwenye nyumba hawezi kukataa kukodisha watu kwa sababu ya asili yao, dini yao, au nchi wanayotoka.



Unapofika Marekani kwa mara ya kwanza, utatumia muda mrefu kutembea kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine. Si muda mrefu utanza kutumia usafiri wa umma, na siku moja utaweza kumiliki na kuendesha motokaa.

Mwanzoni, ukijifunza maana ya alama za uendeshaji wa motokaa na sheria nyingine za barabara, itakuwa rahisi kwako kutumia usafiri wa umma na kujifunza kuendesha motokaa Marekani.

Usafiri wa Umma

Usafiri wa umma ni tofauti kutoka jamii moja hadi jamii nyingine hapa Marekani. Katika miji mikubwa kuna aina tofauti za usafiri kama mabasi, treni za chini kwa chini, na treni za kawaida zinazowawezesha watu kusafiri sehemu zote za mji bila ya kuendesha motokaa. Teksi zinapatikana pia lakini kawa kawaida ni ghali. Sehemu nyingine, usafiri wa umma haupatikani kwa urahisi. Shirika lako la makazi mapya litakupa maelezo kamili juu ya usafiri wa umma kwenye jamii yako mpya mara tu utakapofika.

Kumiliki na Kuendesha Motokaa

Katika maeneo ambayo usafiri wa umma haupatikani au haupatikani kwa urahisi, huenda ukataka kuwa na motokaa yako mwenyewe haraka iwezekanavyo. Kumiliki motokaa ni jambo la kufaa, lakini ni ghali pia. Hali kadhalika, kuna majukumu mengi yanayohusiana na kumiliki na kuendesha motokaa Marekani.

Sheria za wanaomiliki motokaa na waendeshaji motokaa zimewekwa na serikali za majimbo. Shirika lako la makazi mapya linaweza kukueleza sheria za jimbo unalokaa na kukupa maelezo kuhusu mahali ambapo unaweza kupata kibali cha kukuwezesha kujifunza kuendesha motokaa Marekani.

Ili kuendesha motokaa kihalali, ni lazima uwe na leseni ya dereva ya jimbo lako. Leseni ya kuendesha motokaa ya kimataifa haikubaliwi kutumika badala ya leseni ya jimbo. Ukiendesha motokaa bila ya leseni, unaweza kutozwa faini au kupelekwa jela. Ni lazima uwe na umri fulani ili uweze kuendesha motokaa; umri ni tofauti kutoka jimbo moja hadi jimbo jingine.



Kupata leseni, lazima uende Idara ya Motokaa ya mahali unapokaa (Department of Motor Vehicle [DMV]) na upimwe macho, na ufanye mitihani miwili: mtihani wa kuandika juu ya sheria na kanuni za uendeshaji motokaa, na mtihani wa kuendesha motokaa. Itabidi ulipe ada unapofanya maombi ya kupata leseni. Leseni yako ya kuendesha motokaa itakuwa na picha yako, jina lako, anuani, na tarehe yako ya kuzaliwa, na ni lazima ufanye leseni mpya kila baada ya miaka fulani.

Kuvunja sheria fulani kutasababisha upoteze leseni yako. Kwa mfano, ukikamatwa unaendesha motokaa ukiwa katika hali ya ulevi, unaweza kupoteza leseni yako, unaweza kulipa faini kubwa, au ukapelekwa jela kwa muda fulani. Unaweza pia kufukuzwa nchini na kurejeshwa nchini ulikotoka.

Baada ya kununua motokaa, ni lazima uiandikishe kwenye DMV iliyoko sehemu unayokaa na ikaguliwe kuhakikisha kwamba ni salama kuendesha motokaa hiyo. Ni lazima pia uwe na bima ya motokaa hiyo. Bima hutolewa na makampuni ya bima ya binafsi. Gharama za bima za motokaa zinategemea sehemu unayokaa, umri wako, watu wangapi watakuwa wanaendesha motokaa hiyo, na historia yako ya uendeshaji. Itabidi uzingatie gharama za kuweka gesi, uangaliaji wa motokaa, na gharama za kugesha motokaa.

North America



New York → Los Angeles	(2,911 Miles/4,684 Kilometers)
New York → Chicago	(818 Miles/1,316 Kilometers)
New York → Miami	(1,325 Miles/2,132 Kilometers)



Wamarekani wengi wanaweka thamani kubwa kwenye uwezo wa kujitegemea. Wanaamini kwamba watu wazima lazima wafanye kazi kujiangalia na kuangalia familia zao, na wasitegemee msaada wa fedha kutoka serikalini. Kwa sababu hii, kutafuta kazi ni jambo muhimu la kwanza kwa wakimbizi mnamo miezi yao ya mwanzo Marekani na moja katika malengo yako ya kwanza litakuwa kupata kazi.

Mwanzoni, utategmewa kufanya kazi yoyote ya kwanza utakayopata, hata ikiwa kama hailipi vizuri au si sawa na kazi yako uliyokuwa ukifanya kabla. Wamarekani wengi wanaamini kwamba kuwa na kazi yo yote ni bora kuliko kuwa bila ya kazi.

Serikali au shirika lako la makazi mapya halikuhakikishii kwamba utapata kazi. Huduma za kuajiriwa za wakimbizi zitakusaidia katika juhudi zako za kutafuta kazi, lakini huwezi kupata kazi kama wewe mwenyewe hufanyi juhudi. Kwa vile utakuwa unashindana na watu wengine ambao wanatafuta kazi hizo hizo, itabidi uonyeshe kwamba uko tayari kufanya kazi.

Aina za kazi

Marekani, kuna aina tatu za kazi: kazi za kiwango cha kwanza, kazi za ufundi, na kazi za taalimu au ubingwa. Kwa kila aina ya kazi, mtu anahitaji kuwa na kiwango fulani cha uzoefu au mafunzo.

Kazi za kiwango cha kwanza zinahitaji mafunzo

kidogo au uzoefu mdogo. Mifano ya kazi za aina hii ni wasafishaji hoteli, waandikiaji chakula wa hoteli, na wafanyakazi viwandani. Kazi hizi hulipa mshahara kwa masaa na hazihitaji kiwango cha juu cha ujuzi wa lugha ya Kiingereza. Wakimbizi wengi wanafanya kazi hizi huku wanasoma Kiingereza au kujifunza ujuzi mwingine.

Kazi za ufundi zinahitaji mafunzo, kiwango cha juu cha ujuzi wa lugha ya Kiingereza, na kiwango fulani cha ujuzi wa kazi hiyo. Fundi wa motokaa, mfanyakazi wa urembo, fundi umeme, fundi wa kompyuta ni mifano ya kazi za



ufundi. Kazi za ufundi zinalipa mshahara, kwa masaa au kwa wiki, ambao ni mkubwa kuliko mshahara wa kazi za kiwango cha kwanza, na ni mkubwa hata kuliko kazi za taalimu au ubingwa. Kazi nyingi zinazohitaji ujuzi zinataka wafanyakazi wawe na shahada au wawe wanachama wa chama cha wafanyakazi fulani. Shahada kutoka nchini kwako huenda zisikubaliwe, lakini unaweza kusoma Kiingereza na ukachukua masomo ambayo yatakuwezesha kupata shahada ya Marekani katika uwanja wako wa kazi.

Kazi za taalimu au ubingwa Kwa kawaida zinahitaji shahada ya chuo kikuu, kiwango cha juu cha Kiingereza, na ujuzi wa juu katika kazi yako. Kupata ujuzi katika mambo hayo matatu huchukua muda mrefu. Vile vile, kazi nyingi za ubingwa, kama kazi za udaktari au kazi za kufundisha, huhitaji upate leseni au shahada kwenye jimbo unakofanya kazi. Hata kama una shahada kutoka nchini kwako, mafunzo ya ziada na mitihani ya kupata shahada tena itatakiwa kabla ya kuanza kazi Marekani. Kazi za ubingwa nyingi zinatoa mshahara, hii ina maana kwamba mshahara umewekewa kiwango maalum cha mwaka, badala ya malipo kwa masaa.

Wanawake na Wanaume Kazini

Marekani, wanawake na wanaume, wote wanafanya kazi. Nusu ya wafanyakazi ni wanawake, na wanafanya kazi sawa na wanaume na kwenye viwango vyote vya kazi, na mara kwa mara husimamia wafanyakazi wa kiume. Jambo hili linaweza kuwa tofauti na desturi zinazofuatwa nchini kwako, na labda hujazoea kuona wanawake wanafanya kazi nje ya nyumba zao. Lakini kuna faida kubwa ikiwa wazazi wote wawili wanafanya kazi, kwa sababu kuwa na vipato viwili kutasaidia familia kupata maendeleo haraka zaidi na kujitegemea kifedha. Watoto wenye umri zaidi ya miaka 15 wanaweza kufanya kazi za muda, na vijana wengi Marekani hufanya kazi za muda jioni baada ya shule, siku za wikendi, na wakati wa likizo.

Kutafuta kazi

Kujitahidi na kuvumilia kwako kutakusaidia katika kupata kazi. Lakini, kuna huduma nyingine za kukusaidia katika juhudi zako.

Mashirika ya makazi mapya na huduma za

kuajiri wakimbizi. Wafanyakazi wa mashirika ya makazi mapya na huduma za kuajiri wakimbizi wamewasaidia wakimbizi wengi kupata kazi zao za kwanza Marekani. Waambie maoni yako, na sikiliza ushauri wao. Watakusaidia kuelewa aina ya kazi ambayo unaweza kutaraji kupata kwa kutegemea ujuzi wako na uzoefu wako wa kazi.

Mashirika ya ajira ya umma. Kila jimbo lina mashirika ya ajira ya umma ambayo yanaweza kukusaidia bila ya kukulipisha ada. Shirika lako la makazi mapya litaweza kukwambia ofisi hizo ziko wapi.

Marafiki na jamaa. Marafiki, jamaa, wakimbizi wengine katika jamii ambao wamefika kabla yako wanaweza kukwambia kama kuna nafasi za kazi wanakofanya kazi au kwenye sehemu nyingine wanazozijua.

7 among the
t the original
t of 6.375%
1 broken will
those for the
s. Annapolis,
that property

NUMBER 17,
ON A PLAT
IN THE LAND
ING IN PLAT
BEING
NO. 21122.

the amount of
old in '86. It
ditions, liens,
ams, if any,
verified funds
the purchase
date of sale to
after the final
public charges
of the date of
cable, condome-
ments that
sponsibility of
state revenue
needs incident
new as of and

OCTOBER 1, 8, 15, 2004

L77814

HELP WANTED
900-999

903 Career Training & Employment Services
905 Jobs
927 Domestic
932 Education
941 Healthcare—General
944 Healthcare—Nursing
983 Tech
993 Part-time
993 Positions Wanted—Domestic
995 Positions Wanted

Career Training and Employment Services

BARTEND
5,248 Placement and Metro: 905, 203-841-8700, 2448 Wilson Blvd, Ar

A JOBS
Accounting-Admin
PT Administrative position with Accounting experience. Must have good relationship with insurance companies. Must have good as well as recruit, manage and motivate all personnel.

A JOBS
ADDS MANAGERS
Up to \$15/hr. No exp. nec. Will train. 7:30-11:00
Must be 18+. 301-484-9700

AUTO
ASM
High vol. dealer in Rockville looking for experienced ASM. This is a full opportunity to join our team at a station of fun and loyalty. Candidates must be energetic, detail oriented, and possess first rate customer skills. Only top-producers need apply. No pay and benefits. Call Jeremy Finkett at 301-269-2053.

AUTO BODY SHOP MANAGER
Excellent opportunity for individual with high volume body shop management experience. Must have good relationship with insurance companies. Must have good as well as recruit, manage and motivate all personnel.

SCHEDULE:
Do you coach a team that requires assignments left? Does your car cause a problem with your work schedule? Is a two-day assignment not enough for your lifestyle? System Part has your answer. We are open to new hires to manage with confidence to suit your needs. Good technicians in short supply. If you qualify you can earn big wages and benefits and still have the lifestyle you desire. We have openings for car and truck technicians. This is not an overnight. Our technicians have been working these schedules for years.
Call Mike O'Connell or Paul O'Connell at 703-448-6966.

AUTOMOTIVE
Expanding MSB Sales team has immediate openings for an experienced Salesperson. Good CMA program track record. Ability to multi-task must be organized and able to schedule and plan. After successful interview, services required. For consideration, please forward resume to: 571-434-2400 ext. 1117 or email resume to: jimb@msbsales.com.

Magazeti mengi ya Marekani yana sehemu za matanzazo zinazoorodhesha kazi zinazoweza kupatikana kama “Msaada Unatakiwa” au “Kuajiriwa”

Magazeti. Magazeti mengi yanaorodhesha kazi zinazoweza kupatikana kwenye sehemu inayoitwa “msaada unatakiwa.”

Mashirika binafsi ya ajira. Mashirika binafsi ya ajira yanalipisha ada kukusaidia kupata kazi. Baadhi ya ada hizi ni kubwa, na inabidi uhakikishe kuwa umeelewa kanuni zao kabla ya kuweka sahihi kwenye mkataba. Kama huelewi, omba msaada kutoka shirika lako la makazi mapya.

Utunzaji wa Watoto

Kama wewe ni mzazi bila ya mume au mke, au ikiwa wewe na mume wako au mke wako nyote wawili mnafanya kazi, utahitaji kutafuta mtu kutunza watoto wako wakati uko kazini. Kwenye baadhi ya familia za wakimbizi, mtu mzima mmoja ambaye hafanyi kazi huangalia watoto, au wazazi wanatafuta kazi zenye ratiba tofauti ili aweko mzazi mmoja nyumbani wakati wote.

Jamii nyingi hutoa huduma za kutunza watoto, lakini kwa kawaida kuna ada za kulipa. Watu binafsi wanaweza kutoa huduma za kutunza watoto majumbani mwao. Wafanyakazi wa shirika lako la makazi mapya wanaweza kukupa ushauri juu ya huduma za utunzaji wa watoto katika jamii yako.



Utatakiwa uonyeshe ushabidi kwamba una ruhusa ya kufanya kazi. Wakimbizi wengi wanatumia kadi ya I-94 (ilyowekewa muhuri na CIS ya kukuwezesha kufanya kazi), kadi ya dhamana ya jamii (Social Security), na kitambulisho chenye picha kama nyaraka za kukuwezesha kufanya kazi (Employment Authorization Document, EAD), pasipoti ya safari, au leseni ya kuendesha motokaa. Lazima uwe na nakala asili ya nyaraka hizi ukienda kwenye mahojiano ya kazi; kopi za nyaraka hazikubaliwi.



Mashauri Ili Upate Mafanikio kwenye Mahojiano ya Kazi

Mara utakapotambua waajiri gani wataweza kukuajiri, ni lazima ufanye mahojiano ya kazi. Mtu atakayekuhoji atakupua maelezo ya kazi na atazungumza nawe ili ahakikishe kama utakuwa mfanyakazi mzuri. Unaweza kufanya mambo yafuatayo ili uonekane kwamba utakuwa mfanyakazi mzuri:

Fika bila ya kuchelewa. Kufuata saa ni muhimu sana kwa Wamarekani. Ukichelewa kwa miadi ya mahojiano, mkuu wa kazi atafikiri kwamba utachelewa kila siku kufika kazini pia.

Kuwa msafi na kuvaa mavazi yanayokubalika kikazi. Anayekupa ushauri juu ya kuajiriwa anaweza kukusaidia kuhusu aina ya mavazi unayoweza kuvaa.

Mtazame anayekuhoji machoni, mshike mkono huku ukitabasamu. Katika baadhi ya nchi kumtazama mkubwa wa kazi machoni kunaonekana kama ni tabia mbaya, lakini Wamarekani wanaamini kwamba kumtazama mtu machoni kunaonyehsa uaminifu, na kutabasamu na kumshika mtu mkono kunaonyesha tabia nzuri ya kazi.

Uliza maswali kuhusu unayotarajiwa kufanya kazini. Kuuliza maswali kutamwonyesha atakayekuhoji kwamba unapenda kazi.

Jaribu kuondoa wasi wasi. Kwa kawaida watu huwa na wasi wasi wakati wa kufanya mahojiano ya kazi. Tambua kwamba wewe huko pekee katika jambo hili.

Huenda ikabidi ufanye mahojiano kadhaa ya kazi kabla ya kuajiriwa. Hili ni jambo la kawaida kwa watafutaji kazi wote Marekani. Huenda ukavunjika moyo kama hukuajiriwa baada ya mahojiano yako ya kwanza, lakini jaribu kuwa na subira.



Zungumza na familia yako na mshauri wako wa kuajiriwa kama unataka msaada wa kupata moyo zaidi wa kuendelea.

Malipo, Makato ya Kodi, Makato ya Hiari, na Mafao

Utakapopewa kazi, mwajiri atakwambia malipo yako yatakuwa kiasi gani, kama utalipwa malipo ya masaa au utalipwa mshahara wa mwaka, mafao gani yanapatikana, mara ngapi utalipwa, masaa mangapi kwa wiki unatarajiwa kufanya kazi, na ratiba ya kazi ikoje. Kama huelewi kitu, uliza.

Utakapo pokea malipo yako kwa kufuata ratiba iliyowekwa ambayo labda ni mara moja kwa wiki, mara moja kila wiki mbili, au mara moja kwa mwezi. Utakapokea malipo yako kama hundi la malipo pamoja na karatasi ya maelezo ya malipo. Karatasi ya maelezo ya malipo itakuwezesha kuwa na historia ya malipo yako, ihifadhi karatasi hii unapopata fedha kutoka hundi lako au unapoziweka fedha benki. Karatasi ya maelezo itaonesha malipo yako jumla kwa kipindi ulichofanya kazi, makato na malipo ya kodi, pamoja na mshahara taslimu.

Malipo ya ujumla (Gross pay) ni jumla ya pesa ulizopata kwa kipindi cha malipo. Jumla ya pesa inapatikana kwa kuzidisha idadi ya masaa uliyofanya kazi kwa malipo yanayotolewa kwa saa moja.

Kodi za mapato (Taxes) zitatolewa na mwajiri wako kutoka hundi lako la malipo yako kabla hujalipokea. Kodi hizi ambazo zinatolewa kutoka hundi lako zinaitwa *makato ya kodi* (*withholding*). Utakapoanza kazi yako, mwajiri wako atakuomba ujaze fomu itakayoripoti malipo unayopata kwenye shirika la serikali linalokusanya kodi (Internal Revenue Service [IRS]). Fomu inamweleza mwajiri ni lazima akate kiasi gani kutoka malipo yako. Kisheria kukatwa fedha ni lazima. Fedha zinazokatwa ni pamoja na huduma za jamii (Social Security) na huduma za afya (Medicare) (baadhi ya wakati inaitwa FICA), kodi ya mapato ya serikali (federal income tax), na katika baadhi ya majimbo, kodi ya mapato ya jimbo. Idadi ya fedha zinazokatwa kwa kila kipengele inaonekana kwenye karatasi ya maelezo ya malipo.

Makato ya hiari (Deductions) ni fedha nyingine zinazokatwa kutoka malipo yako ya ujumla. Unachagua makato gani yatolewe kwa kuzingatia mahitaji yako na mwajiri wako anatoa mafao gani. Kwa kawaida waajiri wanatumia makato kulipia bima ya afya, ada za chama cha umoja wa wafanyakazi, bima ya maisha, au mpango wa kampuni wa kustaafu.

Malipo halisi (Net pay) ni malipo unayopata baada ya kutolewa makato ya kodi na makato ya hiari.

Mfumo wa malipo Marekani unaweza usifahamike vizuri. Kama kuna kitu ambacho hukielewi kuhusu hundi lako la malipo au karatasi ya maelezo ya malipo, omba msaada kutoka kwa mtu anayekupa ushauri wa ajira au wafanyakazi wa shirika lako la makazi mapya.

Pamoja na malipo unayopata, mwajiri wako huenda akatoa mafao mengine kama bima ya afya. Baadhi ya waajiri hutoa bima ya afya bila ya kuwatoza waajiriwa pesa; wengine huwataka



waajiriwa wao watoe sehemu ya gharama ya bima ikiwa kama sehemu ya makato. Kwenye baadhi ya makampuni, waajiriwa wanapata manufaa ya bima ya afya baada ya kuajiriwa kwa muda, kama miezi 3 au miezi 6.

Gharama za kulipia huduma za afya Marekani ni kubwa sana, kwa hivyo ni muhimu sana kuzingatia bima ya afya wakati unapotafuta kazi. Itakuwa jambo la busara kufanya kazi yenye malipo ya chini lakini inatoa bima ya afya kuliko kufanya kazi yenye malipo ya juu bila ya bima ya afya.

Mwajiri wako anaweza kuwa na mafao ya ziada kama likizo ya ugonjwa, muda wa mapumziko, au mpango wa kustaafu. Kwenye baadhi ya ajira, mafao huenda yakaongezeka ukifanya kazi kwa muda mrefu.

Kisheria kuna mafao matatu mengine yanayopatikana yanayohusika na ajira:

Huduma za jamii (Social Security) ni programu ya serikali ya nchi ambayo inasaidia wastaafu. Kiwango cha fedha anazopata mtu kinategemea historia ya pato la huyo mtu hapa Marekani. Ni wafanyakazi waliochangia kupitia



makato ya kodi kwa miaka 10 au zaidi ndio wanapata mafao ya huduma za jamii (Social Security).



Bima ya kutoajiriwa ni programu inayoendeshwa na serikali ya jimbo huwapa mafao watu waliopoteza kazi bila ya hiari yao kama kufungwa kwa kampuni.

Fidia ya wafanyakazi huwapa wafanyakazi walioumia wakati wako kazini kiasi fulani cha mshahara na bima ya afya. Programu hii huendeshwa na serikali za majimbo.

Kazi Zinazolipa Fedha Taslimu

Kufanya kazi na kulipwa fedha taslimu ni kinyume cha sheria Marekani kwa sababu kwa kawaida inamaanisha kwamba hulipi kodi za mapato. Kama mwajiri wako anakulipa pesa taslimu na hakupi karatasi yenye maelezo ya malipo inayoonyesha malipo ya ujumla, fedha zilizokatwa, na malipo halisi, nyote wawili, wewe na mwajiri wako, mnavunja sheria.

Unapolipa kodi ya mapato, unajiwezesha kupata mafao kama mafao ya huduma za jamii (Social Security), fidia ya wafanyakazi, na mafao ya kutokuwa na ajira.







Unapopata fedha taslimu kwa kufanya kazi na usipolipa kodi, una kosa la kukwepa kulipa kodi. Ukikamatwa, itabidi ulipe faini au uende jela. Huenda ukafukuzwa nchini pia.

Haki za Mahali pa Kazi

Kama mkimbizi, una haki za mahali pa kazi sawa na haki alizo nazo raia wa Marekani. Mwajiri hawezi kukubagua kwa sababu ya hali yako ya kuwa mkimbizi na hawezi kukunyima kazi wala kutokukupandisha cheo kwa sababu ya umri wako, rangi yako, ulemavu ulionao, hali ya kuwa au kutokuwa na ndoa, nchi unayotoka, asili yako, dini, au jinsia. Lakini, baadhi ya kazi kama vile kazi nyingi za serikali ya nchi huajiri raia wa Marekni tu. Sheria za ajira zinawalinda wafanyakazi kutokana na hali isiyo ya salama kwenye maeneo ya kazi na pia hali ya ubaguzi na unyanyasaji wa kijinsia.

Historia ya Kazi na Malengo ya Kazi

Kazi yako ya kwanza itakuwa hatua muhimu ya kwanza ya kujiwekea historia ya kazi Marekani. Jaribu kubaki kwenye kazi yako ya kwanza kwa muda wa miezi 6 au zaidi, hata kama hiyo kazi haikuridhishi kitaalimu kama unavyotaka, kwa sababu waajiri wa baadaye wataangalia utendaji wako wa kazi kwenye kazi yako hii ya kwanza wanapozingatia kukuajiri.

Inabidi ujiwekee malengo ya ajira na utambue mambo utakayobidi kufanya ili ufanikiwe kupata malengo hayo. Kupata kazi bora zaidi yenye malipo makubwa zaidi itabidi uimarisha uwezo wako wa lugha ya Kiingereza na huenda ikakubidi kujifunza ujuzi mpya. Kuajiriwa kwenye kazi ya taalimu yako ya kabla, huenda ikakubidi kuhudhuria madarasa na kupata shahada. Anayekupa ushauri wa ajira anaweza kukusaidia kuunda mpango wa kukuwezesha kufikia malengo yako.

Labda itabidi ufanye kazi tofauti kadhaa kabla ya kufikia lengo lako la mwisho. Hili ni jambo la kawaida Marekani, Wamarekani wengi wanabadilisha kazi mara kadhaa katika miaka yao ya kazi. Huenda ukachukua muda mrefu kufikia malengo yako, na itabidi uwe na subira. Zaidi ya yote, kumbuka kwamba Marekani inajulikana kuwa ni nchi yenye nafasi kwa wale wenye jitihada ya kazi.

Mambo ya Kuzingatia Ili Ufanikiwe Katika Kazi

Mashirika ya makazi mapya na wakimbizi wengi wanasema kwamba mambo yafuatayo yatakusaidia kupata kazi yako ya kwanza na kupata kazi bora zaidi baadaye.

Nenda kazini bila ya kuchelewa. Waajiri wanathamini mtu anayewahi kufika kazini, na utakuwa na sifa nzuri ikiwa daima unafika kazini bila ya kuchelewa. Ukichelewa kufika kazini, malipo yako huenda yakapunguzwa.

Chukua likizo ya ugonjwa unapokuwa mgonjwa tu. Wamarekani wengi huendelea kwenda kazini hata kama wanaumwa kidogo, na wengi huwa na fahari ikiwa hawakukosa kazi kwa sababu ya kuumwa.

Piga simu ikiwa huwezi kwenda kazini. Daima mpigie simu mkuu wako wa kazi ikiwa utachelewa kufika kazini au hutaweza kufika kazini kwa sababu yoyote.

Kuwa mcheshi. Wakati wa chakula cha mchana na muda wa mapumziko unaweza kupata wakati mzuri wa kukutana na wafanyakazi wenzako. Mada za kawaida za mazungumzo hapa Marekani ni pamoja na hali ya hewa, shughuli za wikendi, chakula, na riadha. Kutakuwa na nafasi nyingi za kuzungumza na wafanyakazi wenzako juu ya utamaduni wako hasa wakati wa likizo za kitamaduni.

Chapa kazi ukiwa kazini. Wakati wa kazi, epuka kufanya mazungumzo ya binafsi pamoja na jamaa, rafiki, na wafanyakazi wenzako na kupiga simu au kupokea simu binafsi.

Uliza maswali. Kama kuna kitu hukielewi, uliza. Utafanya kazi vizuri zaidi na mwajiri wako atakuheshimu kwa jitihada yako ya kujifunza na kujiendeleza.

Jifunze ujuzi mpya na majukumu mapya kila iwezekanapo. Unaweza kupata kazi bora zaidi ukionyesha kwamba uko tayari kuchukua majukumu zaidi.

Kabla ya kuacha kazi toa taarifa. Unapoacha kazi moja ili uchukue kazi nyingine, mwarifu mwajiri wako wa zamani si chini ya wiki 2. Usiache kazi kabla ya kupata kazi nyingine.



Marekani, elimu inapatikana kwa wote bila ya kuzingatia umri wa mtu, asili yake, dini yake, au tabaka lake katika jamii. Wamarekani wengi wanaiona elimu kama njia ya kuwawezesha kupata kazi zinazoridhisha bora zaidi na zinazoweza kuendeleza maisha yao.

Elimu ya umma kwa watoto

Elimu ya umma ni bure na ni lazima kisheria kwa watoto wote wenye umri baina ya miaka 6 hadi 16 kupata elimu. Kwa kawaida watoto wenye umri baina ya miaka 5 hadi 18 wanaweza kupata elimu ya bure ya umma, kutegemea kanuni za eneo la shule la mahali unapokaa. Wazazi wanaweza kuwaandikisha watoto wao kwenye shule za binafsi, lakini ada za shule binafsi kwa kawaida ni ghali.

Kwenye shule za umma za Marekani, watoto wenye asili, dini, na hali ya uchumi tofauti wanasoma na kuwasiliana pamoja madarasani na kwenye shughuli za nje ya madarasa. Karibu shule zote za umma, wavulana na wasichana wanafundishwa pamoja kwenye darasa moja. Watoto wenye ulemavu wa mwili au wa kiakili lazima wahudhurie shule pia. Katika hali hizi, shule inatathmini ulemavu wa mtoto na kujadiliana na wazazi mpango wa elimu ya mtoto huyo.

Kuna viwango vitatu vya elimu katika Marekani. Madarasa yaliyoko kwenye kila kiwango huwa tofauti kutoka eneo la shule moja kwenda jingine.

Shule ya msingi huanza na darasa la chekechea (miaka 5) na huendelea mpaka darasa la 5 au darasa la 6 (miaka 12).

Shule ya sekondari ya kati kwa kawaida ina madarasa kutoka darasa la 6 mpaka la 8.

Shule ya sekondari ya juu kwa kawaida huwa na madarasa kutoka darasa la 9 mpaka la 12, mpaka umri wa miaka 18. Wanafunzi wanaofaulu shule ya sekondari ya juu hupata diploma ya shule ya juu.



Mwaka mpya wa masomo kwenye kila kiwango cha elimu huanza mwisho wa mwezi wa Agosti au mwanzo wa mwezi wa Septemba na humalizika mwisho wa mwezi wa Mei au mwanzo wa mwezi wa Juni. Wanafunzi huhudhuria madarasa kwa muda wa masaa 6 kila siku, Jumatatu mpaka Ijumaa. Wanafunzi ambao wanahitaji msaada kujiendeleza katika masomo yao huenda ikabidi wahudhurie shule ya kiangazi mwezi wa Juni na mwezi wa Julai.

Mara tu baada ya kufika Marekani, lazima watoto waandikishwe kwenye shule. Shirika lako la makazi mapya litakusaidia kuwaandikisha watoto wako. Watawekwa kwenye darasa kwa kufuatana na umri wao na madarasa waliyosoma kabla, ijapokuwa mwanzoni watoto wadogo wasiojua Kiingereza huenda wakawekwa kwenye madarasa ya chini zaidi.

Shule zinahitaji kadi za chanjo za kinga za mtoto na historia yake ya afya. Kama huna nyaraka hizi, au kama mtoto hajapata chanjo za kinga bado, shirika lako la makazi mapya litakusaidia kufanya miadi ya kumpatia mtoto chanjo hizo.

Kuhudhuria shule ni muhimu sana. Watoto wasipohudhuria shule wanatarajiwa walete shuleni barua ya maelezo, na wanafunzi wanatarajiwa kufanya kazi za shule walizozikosa.



Ijapokuwa elimu ya umma ni bure, wazazi wanalipa gharama fulani kama vile gharama za mahitaji ya shule na ada kwa shughuli maalum. Kama shule iko mbali na nyumbani na mtoto hatoweza kutembea, mabasi ya shule huenda yakatoa usafiri wa bure wa kwenda shule. Watoto wanaweza kuleta shule chakula chao cha mchana au wanaweza kununua chakula cha lishe nzuri cha mchana kwa gharama ya chini kwenye kafeteria ya shule.

Hakuna mwongozo wa masomo wa taifa katika Marekani; mifumo ya shule ya kila jimbo na kila mji huamua masomo gani yafundishwe shuleni. Kwa ujumla, wanafunzi husoma Kiingereza, hesabu, masomo ya jamii, sayansi, na elimu ya mwili. Sanaa, muziki, na lugha za kigeni hufundishwa pia. Shule nyingi, hasa shule za sekondari za juu, huwa na michezo ya riadha na shughuli za vilabu wakati wa masaa ya shule na baada.

Mtindo wa kufundisha wa Marekani huenda ukawa tofauti sana na mtindo wa kufundisha katika nchi yako. Walimu wanawahimiza wanafunzi wajifunze kwa kufikiri na kuchambua zaidi kuliko kujifunza kwa moyo. Wanafunzi wanashiriki darasani kwa kuuliza maswali na kwa kujiunga kwenye majadiliano na shughuli tofauti, hata kama hawazungumzi Kiingereza vizuri.



Tatizo moja kubwa kwa wanafunzi ni kujifunza Kiingereza. Watoto wadogo wanajifunza kwa haraka, lakini watoto wakubwa huchukua muda mrefu zaidi. Shule nyingi zina madarasa ya kusoma Kiingereza kama lugha ya pili kwa wanafunzi wapya; shule nyingine zinatoa msaada kupitia mwalimu maalum au mkufunzi. Wanafunzi wapya wengi wanakabiliana na matatizo ya kujirekebisha katika mwaka wao wa kwanza. Watoto huenda wakajiona wapweke mwanzoni, lakini kama uwezo wao wa kuwasiliana unavyoendelea vizuri, huweza kufanya marafiki na kujihisi vizuri shuleni.

Wanafunzi wengi wapya na wazazi wao wanastaajabu kuona tabia isiyo rasmi na mavazi yasiyo rasmi ya wanafunzi wa Marekani. Shule za umma za Marekani zinawapa wanafunzi uhuru wa kuchagua kufanya mambo wanayotaka, lakini wanatarajiwa pia kufuata sheria za shule. Wakivunja sheria, wanafunzi huenda wakapewa kazi zaidi za nyumbani, au kufukuzwa shule kwa muda wa siku chache. Kupiga wanafunzi hakuruhisiwi kwenye shule za Marekani.

Baadhi ya shule, hasa shule kubwa katika miji mikubwa, zina matatizo ya kuwa na magengi ya vijana na ugomvi baina ya vikundi vyenye asili tofauti. Kwenye baadhi ya maeneo, kumetokea matatizo ya wanafunzi kutumia madawa ya kulevya na kuleta silaha shuleni. Kama watoto wako watashtuka



au watabaika, itabidi wajaribu kuepuka mashindano na wazungumze na mwalimu, mtoaji ushauri wa wanafunzi wa shule, au mkufunzi.

Walimu na watu wanaohusika na elimu nchini Marekani wanaamini kwamba ni lazima wazazi wajishughulishie katika elimu ya watoto wao kwa sababu kufanya hivyo kunasaidia watoto wafaulu shuleni. Shule zinajaribu kuwasaidia wazazi waelewe elimu ya watoto wao, na shule nyingi hutoa maelezo hasa kwa wazazi wasiozungumza Kiingereza. Mara mbili kwa mwaka, shule zitakutana na mwalimu mzungumze juu ya maendeleo ya watoto wako. Wewe pia unaweza kuomba ukutane na walimu wa watoto wako wakati wowote unapokuwa na maswali au wasi wasi. Unaweza pia kuhudhuria mikutano ya shule, hata kama huzungumzi Kiingereza sana.

Elimu Kwa Watu Wazima

Wamarekani wengi wanaiona elimu kama jambo linaloendelea maishani, na wengi hujiandikisha kwenye masomo wakati fulani kwenye maisha yao ya utuuzima. Baada ya kuamua kuendelea na masomo yao, watu wazima wengi wanaendelea kufanya kazi zao na huku wanahudhuria madarasa jioni au siku za wikendi yaani Jumamosi na Jumapili.

Wakimbizi, pia, wanaweza kuendelea na masomo yao huku wakifanya kazi. Shirika lako la makazi mapya linaweza



kukusaidia kutafuta nafasi za kusoma katika jamii yako, kutoka madarasa ya Kiingereza kama lugha ya pili na masomo ya kupata diploma ya shule ya sekondari ya juu hadi madarasa ya mafunzo ya ufundi na taalimu. Mara tu baada ya kutulia vizuri kwenye makazi yako mapya katika jamii, utajifunza zaidi juu ya nafasi za masomo zinazopatikana. Labda utakuwa na nafasi ndogo ya kupata elimu ya juu katika mwaka wako wa kwanza Marekani. Lakini baadaye unaweza kuamua kuendelea kusoma kupata shahada ya juu au kupata shahada ya taalimu yako. Ni muhimu kwa familia kushirikiana kupanga vipi watu wazima katika familia wanaweza kupata elimu na vipi wanaweza kupata fedha za kugharimia elimu hiyo.

Zifuatazo ni nafasi chache za kupata elimu ambazo unaweza kuzipata katika jamii yako:

Madarasa ya Kiingereza kama lugha ya pili na madarasa ya kusoma na kuandika. Jamii nyingi hutoa madarasa ya Kiingereza kupitia programu za elimu kwa watu wazima kwenye vyuo vya jamii, na shule za sekondari ya juu. Watu wote wanaweza kusoma madarasa haya ijapokuwa mengine huenda yakatoza ada ndogo za masomo. Baadhi ya mashirika binafsi na mashirika yasiyokuwa ya faida, kama mashirika ya makazi mapya, na mashirika ya MAA, hutoa pia masomo ya Kiingereza kama lugha ya pili.



Madarasa haya kwa kawaida ni bure, lakini huenda yakawa na watu wengi wanaosubiri kujiunga. Shule za lugha za pesa pia hutoa masomo ya Kiingereza, lakini kwa kawaida shule hizi ni ghali. Kusoma pamoja na mwalimu msaidizi anayejitolea ni njia nyingine ya kujifunza Kiingereza, na inaweza kuwa njia nzuri ya kujifunza kuhusu utamaduni na mila za Wamarekani.

Kwenye madarasa ya Kiingereza kama lugha ya pili, wanaume na wanawake wenye umri tofauti, na wenye elimu na asili tofauti huhudhiria madarasa ya Kiingereza pamoja. Kwenye kiwango cha kwanza cha madarasa ya Kiingereza, wanafunzi kwa kawaida husoma Kiingereza ili waweze kuwasiliana na watu katika jamii na mahali pa kazi. Kwenye madarasa ya viwango vya juu, wanafunzi hujifunza zaidi sarufi ya lugha ya Kiingereza pamoja na kusoma na kuandika.

Kwenye madarasa ya kusoma na kuandika, wanafunzi hujifunza mambo ya msingi ya kusoma na kuandika pamoja na kujifunza kuzungumza kwa Kiingereza. Kwa sababu kusoma na kuandika ni muhimu katika maisha ya Marekani, madarasa ya kusoma na kuandika huweko kwenye sehemu zile zile zenye madarasa ya Kiingereza kama lugha ya pili na aina nyingine za masomo ya watu wazima. Shirika lako la makazi mapya linaweza kukupa maelezo yanayohitajika.

Madarasa mengine ya watu wazima. Programu za elimu kwa watu wazima hutoa madarasa mengi tofauti kwa watu wa jamii kwa jumla. Masomo haya ni pamoja na masomo ya uwekaji hesabu na akaunti, ujuzi wa kuwa karani, ujuzi wa kompyuta, na lugha za kigeni. Wanafunzi wenye ujuzi mdogo wa Kiingereza hawawezi kusoma kwenye madarasa haya, na wanaoshiriki lazima walipe ada.

Diploma ya kujiendeleza elimu (General Educational Development (GED)). Ili uweze kupata kazi ya juu zaidi, kwa kawaida watu wazima wanahitaji diploma ya shule ya sekondari ya juu. Wakimbizi wenye umri uliopindukia miaka 21 na hawakupata elimu ya shule ya sekondari nchini kwao au hawana diploma wanaweza kusoma ili wapate diploma ya GED. Diploma hii hukubaliwa kuwa sawa na diploma ya shule ya sekondari ya juu.

Shule za ufundi na ustadi. Shule za ufundi na ustadi hufundisha watu kupata kazi zinazohitaji ujuzi maalum, kama makaniki wa motokaa, kufanya programu za kompyuta, na kuwa msaidizi wa daktari au daktari wa meno. Kwa kawaida programu hizi huhitajia kiwango cha juu cha Kiingereza na utaoaji wa ada za masomo. Kwa kazi fulani kama fundi bomba na fundi umeme, wanafunzi hutakiwa wapate mafunzo kwa kufanya kazi yenyewe kabla ya kupata shahada.

Vyuo vidogo na vyuo vikuu. Kuna aina kuu mbili za elimu ya juu nchini Marekani: vyuo vya jamii na vyuo vya miaka minne.

Vyuo vya jamii vinatoa programu za miaka miwili zinazowasaidia wanafunzi kupata taalimu fulani, kama uhasibu au uuguzi. Kwenye baadhi ya taalimu wanafunzi wanaweza kupata shahada mwishoni mwa programu ya miaka miwili ya chuo cha jamii. Kwenye taalimu nyingine, wanaanza kwenye programu ya miaka miwili ya chuo cha jamii na baadaye kujiunga na programu ya miaka minne ya chuo kikuu. Vyuo vya jamii hutoa shahada katika masomo ya ubinadamu, masomo ya sayansi ya jamii, na masomo ya sayansi.

Kwenye vyuo vya miaka minne, wanafunzi huhitajiwa kukamilisha mwongozo wa masomo wa jumla kabla ya kuanza taalimu yao mahsusi kama fizikia, hesabu, au historia, au kujitayarisha kwa masomo ya juu kwenye sheria au udaktari. Vyuo hivi huhitaji viwango vya juu zaidi vya Kiingereza na huhitaji wanafunzi wasiozungumza Kiingereza kama lugha yao ya kwanza wafanye mtihani wa lugha kabla ya kujiandikisha kwenye masomo. Elimu ya juu si bure na inaweza kuwa ghali sana. Vyuo vingi vina ofisi ya msaada wa fedha inayotoa maelezo juu ya mikopo ya wanafunzi na msaada wa fedha wa masomo. Kupata msaada wa masomo utakaolipia masomo yote ni adimu kupata, kwa hivyo ili kuhudhuria chuo kikuu inabidi uweze kujihudumia mwenyewe kifedha.

Watu wenye shahada za juu za udaktari au uhandisi kutoka nchi zao huenda wakahitaji shahada nyingine ya Marekani kabla ya kuruhusiwa kufanya kazi Marekani. Utaratibu wa kupata shahada nyingine unaweza kuwa ghali na unaweza kuchukua muda mrefu. Unahitaji ushahidi wa elimu na sifa zako za elimu kutoka nchi yako, na pia unahitaji kuwa na matokeo halisi ya mtihani wa lugha ya Kiingereza. Wakimbizi wanaotaka kuingia kwenye taalimu zao mara nyingi hufanya kazi ya kiwango cha chini kwenye taalimu hizo wakati wanapojitayarisha kupata shahada nyingine. Kwa mfano, daktari huenda akafanya kazi kama msaidizi wa maabara kabla hajapata rufusa rasmi ya udaktari.



**THE AMERICAN UNIVERSITY
HEALTH INSURANCE CLAIM FORM**

MAIL TO: **EARLY CASBIDY & SCHILING**
4701 Sangamon Road
Bethesda, MD 20814
(301) 273-3400

Continuation Code _____

Phone Number _____ **TO BE COMPLETED BY STUDENT** _____ Social Security No. _____

Student's Name _____ Sex _____ Age _____

Present Address _____

Home Address _____

Causes for absences, sick leave and expenses _____

Date of accident or illness _____

Nature of injury or illness _____

If injury, describe facts how and where accident occurred _____

If injured in auto or operation of auto, indicate other party _____

© 1978 EARLY CASBIDY & SCHILING, INC.



Kukutana kwako kwa mara ya kwanza na huduma za afya za Marekani labda kutakuwa kwenye ukaguzi wa afya wa kwanza. Shirika lako la makazi mapya litakupangia ukaguzi huu mara tu baada ya kufika Marekani. Ukaguzi utatambua na kutibu matatizo yoyote ya kiafya ambayo yanaweza kuingilia shughuli za makazi yako mapya, kama vile uwezo wako wa kufanya kazi au uwezo wa watoto wako kwenda shule. Watoto wako watapata chanjo ya kinga wakati wa ukaguzi kwa sababu watoto wote wanaojiandikisha kwenye shule za umma lazima waonyeshe ushahidi wa kuchanjwa. Ukaguzi wa afya ni bure na kwa kawaida hufanywa kwenye zahanati ya afya, kituo cha afya cha jamii, au ofisi ya daktari.

Baada ya ukaguzi wa kwanza wa afya, utahitaji kuelewa vipi mtapata huduma za afya wewe au jamaa katika familia yako mtakapohitajia. Kufanya hivyo itabidi uelewe vipi Wamarekani wanafikiri kuhusu afya na pia ujue muundo wa huduma za afya Marekani.

Fikira za Wamarekani Juu ya Afya

Wamarekani wanaamini kwamba watu wanaweza kuepuka magonjwa kwa kuwa na usafi, kuwa na lishe nzuri, kufanya mazoezi, na kupata usingizi wa kutosha. Wamarekani wanavaa nguo zinazowafanya wapate joto wakati wa baridi na nguo zinazowasaidia kupunguza hali ya joto wakati wa majira ya joto. Wanakwenda kwa daktari au kwenye zahanati ili kukaguliwa mwaka mara moja, ili waweze kujua wana matatizo gani ya kiafya kabla matatizo hayo hayajawa matatizo makubwa. Wanakwenda kumwona daktari wa meno ili meno yao yasafishwe. Wanaita mambo haya yote mtindo wa maisha wa kiafya.

Muundo wa afya wa Marekani unategemea sana mbinu za sayansi kugundua matatizo ya kiafya na kutibu wagonjwa. Hii ina maana kwamba, pamoja na kuwauliza wagonjwa wanajihisi vipi, madaktari wanafanya ukaguzi kwa kutumia damu au sampuli nyingine kutoka mwilini. Matokeo ya ukaguzi yanamsaidia daktari kuamua vipi kumtibu mgonjwa. Kama huhisi vizuri kutolewa damu au kutoa sampuli nyingine mwilini, zungumza na daktari wako kuhusu hali hiyo.



Madaktari wa Marekani hawana uzoefu wa kutibu magonjwa kutoka nchi nyingine. Huenda ikabidi umweleze daktari wako vipi wewe na watoto wako mmepata matibabu kabla, na umweleze, kwa kawaida, mambo gani ulifanya na dawa gani uliyotumia kushughulikia ugonjwa huo.

Watoaji Huduma za Afya

Marekani, kuna aina tofauti za watoaji huduma za afya. Wafanyakazi wa shirika lako la makazi mapya wanaweza kukwambia aina gani za watoaji huduma za afya wako katika jamii yako na huduma gani wanazotoa.

Idara ya afya ya umma. Kila jimbo lina idara ya afya ya umma yenye ofisi kwenye jamii katika sehemu zote za jimbo. Idara za afya ya jamii zinatoa chanjo za kuingia maradhi na zinatoa huduma nyingi za afya za kuepuka magonjwa, zikiwemo kufanya ukaguzi na kutibu maradhi ya kifua kikuu. Kwa wakimbizi, huduma hizi ni bure au si ghali sana.

Zahanati za jamii na vituo vya afya. Zahanati za jamii na vituo vya afya hutoa huduma za afya za lazima na pia hutoa ushauri wa afya. Baadhi yao hutoa pia huduma za meno na ukaguzi wa macho. Baadhi ya zahanati mijini huangalia wagonjwa mahsusi, kama wanawake waja wazito au watu wenye ukimwi. Zahanati zinapokea bima binafsi



na msaada wa serikali wa afya (Medicaid), na zahanati nyingi hutoza ada kwa kutegemea uwezo wa kulipa wa mgonjwa. Wagonjwa kwa kawaida huhitaji kufanya miadi ili kuweza kwenda kwenye zahanati, lakini baadhi ya zahanati huangalia wagonjwa wanaokwenda bila ya miadi.

Madaktari binafsi. Baadhi ya madaktari hutowa huduma za matibabu ya magonjwa mbali mbali, zikiwemo ukaguzi wa kila mwaka. Wengine wanatoa matibabu kwenye sehemu moja mahsusi ya tiba. Baadhi ya madaktari wanafanya kazi kwenye zahanati ya binafsi au kwenye kikundi cha pamoja na madaktari wengine na madaktari wa magonjwa mahsusi. Mgonjwa lazima afanye miadi kuonana na daktari. Ofisi ya daktari kwa kawaida huhitaji kuona ushahidi wa kulipa au maelezo ya bima wakati unapofika kwa miadi yako.

Madaktari binafsi wa meno. Baadhi ya madaktari wa meno wanatoa huduma za jumla za kuangalia meno, zikiwemo usafishaji na ujazaji mapengo. Wengine wamejihusisha kwenye aina maalum ya matatizo ya meno. Ofisi za madaktari wa meno zinahitaji malipo wakati unapokwenda kwa miadi yako. Mara nyingi bima ya afya hailipi huduma za meno.



Maduka ya madawa au famasia. Haya ni maduka ambayo unaweza kupata dawa ulizoandikiwa na daktari wako, na pia dawa ambazo huhitaji kuandikiwa na daktari kama dawa za kuondoa maumivu. Mtoaji dawa wa famasia anaweza kukupa ushauri kuhusu dawa za kutumia kwa ugonjwa wako na kama unaweza kutumia dawa fulani pamoja na dawa nyingine. Lazima utoe malipo au utoe maelezo ya bima unapopata dawa yako kutoka kwa mtoaji dawa wa famasia.

Hospitali. Madaktari na zahanati huwapeleka wagonjwa wenye matatizo maalum hospitali kufanyiwa mapimo na upasuaji. Huduma kutoka hospitali ni ghali, na hospitali huhitaji ushahidi wa bima au uwezo wa kulipia huduma hizo.

Vyumba vya matibabu ya dharura. Maeneo haya katika hospitali au kwingineko yamewekwa kwa matatizo makubwa ya afya yanayotokea kwa ghafula. Si lazima kufanya miadi kwenda kwenye eneo la hali ya dharura, lakini sehemu hizi ni sehemu zenye shughuli nyingi na utahitaji kusubiri kwa muda mrefu kama hali yako si mbaya sana. Kama tatizo lako si la hali ya dharura, ni bora ufanye miadi ya kwenda kwenye zahanati au ofisi ya daktari. Huduma ya vyumba vya hali ya dharura ni ghali sana.

Huduma za Ambulensi. Huduma hii inatoa msaada wa kiafya na usafiri kwenda kwenye chumba cha hali ya hatari kama hakuna njia nyingine ya kumchukua mjeruhiwa au mgonjwa kupata huduma ya afya ya dharura. Ambulensi hutoza ada baada ya huduma kutolewa.

Utunzaji wa Afya ya Akili

Wamarekani wanaamini kwamba afya ya akili ni muhimu kama afya ya mwili, na miongoni mwa huduma za afya huwemo matibabu yanayotolewa na mtaalamu wa afya ya akili kama ikibidi. Wakimbizi na wageni wengine wanahitaji kuzingatia vizuri afya yao ya akili kwa sababu mara nyingi huwa wamepata hali ya msukosuko wakati wa kukimbia na hali ya kufadhaika wakati wa kujirekebisha na maisha ya Marekani. Kama ukihisi hali yako inakushinda na huwezi kuendelea na shughuli zako za kila siku, ni lazima upatete huduma za afya ya akili. Huduma nyingi za afya ya akili hutolewa na zahanati, madaktari binafsi na wataalamu wengine, lakini baadhi ya huduma za afya ya akili zinapatikana kwa kupitia mashirika ya MAA na mashirika ya huduma za jamii. Baadhi ya mashirika ya makazi mapya yanatoa ushauri, na kukujulisha na vikundi vinavyotoa msaada, au vikundi vya kutoa ujuzi wa kuendeleza maisha, na wanaweza kukusaidia kupata huduma nyingine za afya ya akili.

Kulipia Utunzaji wa Afya

Utunzaji wa afya Marekani ni ghali, na ni watu wenyewe, siyo serikali, wenye jukumu la kulipia huduma za afya. Utunzaji afya ni gharama kubwa, kwa hivyo watu wengi wanategemea programu za bima. Waajiri wengi wanawapa waajiriwa wao programu za bima, na mara nyingi wanalipa sehemu ya gharama ya kila mwezi. Gharama iliyobaki inakatwa kutoka hundi lako la malipo pamoja na kodi zako za mapato, ili usitoe malipo ya ziada. Kwa kawaida kuna muda wa kusubiri kutoka wakati unapoajiriwa mpaka unapoweza kupata bima ya afya.

Mara nyingi waajiri hutoa bima ya afya kupitia mashirika mbalimbali kama la “Health Maintenance Organization (HMO)” au shirika la “Preferred Provider Organization (PPO).” Pamoja na mashirika hayo, vikundi vya madaktari binafsi na zahanati hutoa huduma. Kila anayeshiriki kwenye bima (yaani kila mwajiriwa) hupewa daktari wake. Daktari huyu anamtibu mwajiriwa na lazima atoe ruhusa ya kwenda kwenye vyumba vya hali ya dharura, hospitali, au kumwona daktari mahsus. Kuna baadhi ya huduma ambazo HMO na PPO hulipa gharama zote za utunzaji wa afya anaupata mwajiriwa. Kuna huduma nyingine ambazo mwajiriwa lazima alipe sehemu ya gharama.

Kama mwajiri wako hatoi mafao ya afya, unaweza kununua bima ya afya moja kwa moja kutoka kampuni za bima, HMO au PPO. Wafanyakazi kwenye shirika la makazi mapya wanaweza kukupa ushauri vipi kufanya hivyo.

Kuwasaidia watu wenye mapato ya chini, kuna programu za serikali zinazolipa baadhi ya huduma za afya. Wakimbizi wanaweza kuomba msaada wa huduma za afya kutoka Shirika la Wakimbizi la Msaada wa Afya (Refugee Medical Assistance, RMA) au Msaada wa Afya (Medicaid). Programu zote mbili zinawalipia gharama za huduma za afya watu wenye umri wa kufanya kazi ambao wanapata malipo ya chini, lakini programu hizi zinaweza kutumiwa tu mpaka utakapopata bima kutoka kwa mwajiri wako au utakapoweza kununua bima ya afya mwenyewe. Kuomba msaada kutoka programu hizi, ni lazima ujaze fomu zinazoonyesha ushahidi wa pato lako na maelezo mengine binafsi. Ili uweze kuendelea kupata msaada huu ushahidi hukaguliwa mara kwa mara na maelezo mapya hutakiwa. Madaktari wengi hawakubali aina hizi za bima.

Wakimbizi wenye umri zaidi ya miaka 65 wanaweza kupata msaada wa afya wa Medicare. Hii ni programu ya serikali inayosaidia watu ambao wana umri zaidi ya miaka 65 kulipia gharama zao za huduma za afya. Medicare inalipia sehemu ya gharama za dawa ulizoandikiwa na daktari pia.

Shirika lako la makazi mapya linaweza kukusaidia kuelewa msaada gani wa kulipia huduma za afya ambao unaweza kuupata.

Haki Zako za Kupata Huduma za Afya

Popote unapoishi Marekani, una haki ya kupata huduma za ukalimani na habari zako kuwekwa katika hali ya usiri.

Huduma za ukalimani. Inabidi uwasiliane na umwelewe daktari wako ili uweze kupata matibabu sahihi. Kama ukihisi unahitaji msaada wa lugha kuwasiliana na daktari wako, una haki ya kupata mkalimani akusaidie. Liombe shirika lako la makazi mapya likusaidie kupata mkalimani.

Hali ya usiri. Kisheria kila kinachotokea baina yako na daktari wako huwekwa katika hali ya usiri. Daktari wako hawezi kuwaambia familia yako, rafiki zako, au mwajiri wako kuhusu hali yako ya afya bila kupata kibali chako. Hawezi kuwaambia hata kama una ugonjwa hatari kama ukimwi. Kama una virusi vya HIV au kama una ugonjwa mwingine, ni wewe unayeamua kuwaambia familia yako na marafiki zako. Daktari hawezi kuwaambia mpaka apate kibali chako. Lakini sheria inakutaka umweleze daktari wako juu ya hali yako ya kuwa na virusi vya HIV. Kama humwelezi daktari wako juu ya hali hii, unaweza kupata hukumu kali.



Gharama za kuishi Marekani ziko juu kabisa. Utahitaji kutumia fedha zako kwa uangalifu, ili usitumie fedha zaidi kuliko unavyomudu. Wafanya kazi wa shirika lako la makazi mapya wanaweza kukusaidia kufanya mpango wa matumizi, ili ujue una fedha kiasi gani, unaweza kutumia kiasi gani, na unaweza kuweka akiba kiasi gani.

Kufanya Mipango ya Matumizi

Kila mwezi utahitaji kulipa gharama za maisha ya kawaida na gharama nyingine. Gharama hizi zifuatazo zitakuwa gharama zako kuu.

Kodi ya kupanga. Gharama ya kodi ya kupanga huenda ikawa gharama yako kubwa kuliko gharama nyingine za kila mwezi.

Umeme na gharama nyingine. Hizi ni gharama za umeme, gesi au mafuta, maji, na ukusanyaji wa takataka. Baadhi ya gharama hizi huenda zikawa kwenye kodi yako ya kupanga, lakini huenda ikabidi ulipe gharama nyingine mwenyewe. Gharama za umeme na gesi au mafuta zitakuwa juu wakati wa majira ya baridi utakapohitaji hali ya joto zaidi na wakati wa kiangazi utakapohitaji hali ya baridi zaidi.

Chakula. Unaweza kubana matumizi ya chakula kwa kutafuta maduka na bidhaa zenye bei za chini kabisa.

Utunzaji wa watoto. Utunzaji wa watoto huenda ukawa gharama kubwa ya kila mwezi. Kama huwezi kufanya mpango na jamaa au marafiki kuangalia watoto wako, shirika lako la makazi mapya huenda likaweza kukusaidia kutafuta huduma za utunzaji wa watoto au kuomba msaada wa utunzaji wa watoto.

Usafiri. Usafiri ni pamoja na usafiri wa kwenda kazini na kurudi nyumbani, usafiri wa kwenda madukani, na kwenye miadi. Pasi za bei nafuu za basi au treni hupatikana katika sehemu nyingi.



“*Miaka michache baada ya kufika Marekani, niliamua kuwa umefika wakati wa kununua motokaa.*

Nilipopeleka maombi ya kupata mkopo kwenye ofisi inayouza motokaa, afisa wa mkopo aliniuliza kama nimewahi kupata mkopo kabla.

Nilisema kuwa nimewahi kupata mkopo na nilimwonyesha ushahidi wa mkopo wa IOM ambao nimeshaulipa. Kwasababu nimemwonyesha ushahidi kwamba ninaweza kulipa mkopo, maombi yangu ya mkopo yalikubaliwa.”



Simu. Utahitaji kulipia simu kila mwezi. Kumbuka kwamba kupiga simu za mbali ni ghali.

Mkopo wa safari. Itabidi ulipie mkopo wako wa safari kila mwezi mpaka umalize malipo yote.

Akiba na kusaidia familia yako iliyoko nje ya nchi. Kama una malengo ya muda mrefu kama elimu au kununua nyumba, itakubidi uweke kiasi fulani kwenye akaunti ya akiba ya benki kila mwezi. Huenda ukataka kuwapelekea pesa baadhi ya jamaa zako waliobaki nchini kwenu. Utakapokuwa na kazi na ukajua kuna gharama gani za kila mwezi, unaweza kuamua kiasi gani uweke akiba na kiasi gani upeleke nyumbani kila mwezi.

Utunzaji wa afya. Utakapopata kazi ya kudumu, huenda ukapata aina fulani ya bima ya afya. Lakini kazi nyingi za kiwango cha kwanza hazitoi bima mnamo miezi ya kwanza ya ajira. Huenda ikakubidi ununue bima yako mwenyewe.

Wapi Unaweza Kununua Mahitaji Yako

Maduka na masoko ya Marekani yanatoa aina nyingi za bidhaa na huduma tofauti. Zifuatazo ni aina tano za mahali unapoweza kununua mahitaji yako:

Maduka ya supamaketi. Haya ni aina ya maduka ya kawaida yanayouza chakula. Maduka mengi ya aina hii huuza pia bidhaa za kusafisha, bidhaa za uzuri, magazeti, bidhaa za nyumbani, na dawa zisizohitaji maandishi ya daktari. Watu wengi wanapunguza gharama za chakula kwa kutumia kuponi za kupunguzia bei na kununua bidhaa zenye chapa ya duka au bidhaa ambazo ziko kwenye seli yaani bei zao zimepunguzwa.



Maduka makuu ya bidhaa mbali mbali. Maduka haya huuza fanicha, vifaa mbali mbali vya nyumba, nguo, viatu, na bidhaa nyingine zisizo chakula. Baadhi ya maduka haya ni maduka yanayouza bidhaa kwa bei ya chini.

Maduka ya mitumba na bidhaa zilizotumika. Maduka haya yanauza vitu vilivyokwishatumika kwa bei ya chini vikiwemo fanicha, vitu vya nyumbani, na nguo

Maduka ya vyakula vya asili. Maduka haya humilikiwa na huendeshwa na wahamiaji au wakimbizi waliofika kabla. Yanapatikana kwenye sehemu ambako wakimbizi wengi wanaishi. Huenda ukapata vyakula kutoka nchi yako kwenye duka la vyakula vya asili.

Mauzo yanayofanywa nyumbani. Kwenye mauzo haya, watu wanauza vitu kutoka nyumba zao kwa bei za chini. Ni sehemu nzuri sana za kununua vitu vya nyumbani, fanicha, na nguo. Mauzo ya nyumbani yanatangazwa kwenye magazeti au kwenye matangazo ya mtaani.

Kulipa Kodi

Kodi za mapato Marekani zinalipia huduma nyingi zinazotumiwa na wakazi wote wakiwemo wakimbizi. Kodi za mapato zinalipia elimu ya umma, uangaliaji wa njia na barabara kuu, polisi, huduma za kuzima moto na hali ya dharura, na

programu za huduma za jamii. Watu wanoishi Marekani wanalipa aina tatu za kodi za mapato:

Kodi za mapato. Kila mfanyakazi analipa kodi za mapato ya serikali ya nchi, na wakazi wa baadhi ya majimbo wanalipa kodi ya mapato ya jimbo. Kodi hizi zinatolewa na mwajiri wako kutoka kwenye mshahara wako. Kila mwaka lazima ujaze fomu za kodi za mapato za serikali ya nchi na serikali ya jimbo. Fomu hizi zinaeleza serikali kiasi gani umelipa kama mazuiyo ya ajira, na kama inabidi ulipe zaidi au inabidi urejeshewe fedha na serikali. Shirika lako la makazi mapya litakusaidia kupata fomu za kujaza habari za kodi ya mapato na kukushauri vipi kujaza fomu hizi. Fomu hizi lazima zipelekwe serikalini tarehe 15 Aprili au kabla.

Kodi za mali binafsi. Serikali za miji zinakusanya kodi za mapato za nyumba, ardhi, na majengo unayomiliki. Sehemu nyingine hukusanya kodi kwa kuwa na motokaa.

Kodi za mauzo. Wanunuzi kwenye majimbo mengi wanalipa kodi za mauzo ambazo zinaongezwa juu ya bei ya bidhaa wanayonunua. Baadhi ya bidhaa, kama vyakula au dawa, huenda zisiwe na kodi za mauzo. Kodi hizi ni asilimia fulani ya bei ya bidhaa na huhesabiwa na karani kwenye mashine ya kuhesabia fedha. Bei ya bidhaa fulani inayoonyeshwa kwenye rafu ya duka ni bei ya bidhaa hiyo bila ya kodi ya mauzo.

Huduma za Benki

Kuhifadhi fedha zao, Wamarekani mara nyingi huziweka fedha hizo kwenye akaunti ya benki kuliko kuziweka nyumbani pamoja nao. Fedha unazozuweka benki zimewekewa bima na serikali ya Marekani. Kama fedha hizo zikiibiwa serikali ya Marekani itakulipa.

Benki zina aina tofauti za akaunti kwa madhumuni tofauti. Benki hutoza ada ya kila mwezi kwa baadhi ya akaunti hizi. Kuna aina mbili kuu za akaunti za benki:

Akaunti mbali mbali za akiba. Akaunti hizi ni za kuweka akiba. Benki zinakulipa asilimia fulani ya fedha kwa kuweka fedha zako kwenye akaunti.

Akaunti za hundi. Akaunti hizi hutumiwa kwa kulipa gharama. Benki inakupa hundi unazoweza kuzijaza kulipa kodi ya nyumba na madeni mengine. Ni lazima uchukue tahadhari usiandike hundi za pesa zaidi kuliko ulizo nazo kwenye akaunti yako. Baadhi ya benki zinalipa riba pia kwa kuweka fedha kwenye akaunti ya hundi.

Kutumia Kadi ya Mkopo na Kuweka Historia Nzuri ya Mkopo

Wamarekani kwa kawaida wanatumia kadi za mkopo na mipango ya mkopo kwa manunuzi makubwa kama motokaa, vifaa vya nyumbani, na fanicha. Kwa kutumia kadi za mkopo na mipango ya mkopo, watu wanaweza kununua vitu ghali, kwa sababu wanaweza kulipa kidogo kidogo kwa muda fulani badala ya kufanya malipo yote wakati wa ununuzi.

Unapotumia kadi ya mkopo, unakopa pesa. Benki au kampuni ambayo inatoa kadi ya mkopo inatoza riba juu ya idadi ya pesa ulizokopa, na lazima ulipe kila mwezi. Ukikosa kulipa mwezi mmoja, kampuni inaweza kukichukua kitu ulichonunua kwa mkopo na kukutoza fedha kwa kuchelewa kulipa.

Ukiamua kupata kadi ya mkopo, itabidi uitumie kwa uangalifu. Ni rahisi kupata deni kubwa kwa kutumia kadi za mkopo. Kabla ya kununua kitu kwa kutumia kadi ya mkopo hakikisha kwamba utaweza kufanya malipo ya kila mwezi.

Unapopata mikopo na unapotumia kadi za mkopo unajiweka historia ya mkopo. Mashirika binafsi yanayotoa maelezo ya mkopo yanaweka ripoti ya mkopo inayoonyesha historia ya mkopo, na benki huangalia ripoti hii unapooomba mkopo au kadi ya mkopo. Kama ukifanya malipo kwa wakati kila mwezi, historia yako ya mkopo itakuwa nzuri na benki zitakubali kukukopesha fedha na kukupa kadi za mkopo. Kama ukikosa kulipa au ukitumia kadi yako ya mkopo kupindukia uwezo wako wa kulipa, utakuwa na historia mbaya ya mkopo na hutaweza kupata mikopo au kadi ya mkopo baadaye.

Kwa sababu hii, unahitaji kuweka pesa upande kulipa mkopo wako wa safari kila mwezi. Ni nafasi yako ya kwanza ya kujiweka historia nzuri ya mkopo Marekani. Itakuwa rahisi kupata mkopo baadaye kama ukionyesha kwamba umeweza kulipa mkopo wote kabla. Uliza shirika lako la makazi mapya kuhusu maelezo ya kulipa mkopo wako wa safari.

Hali kadhalika unahitaji kulipa kodi yako ya kupanga na gharama za umeme na gesi au mafuta kila mwezi. Kama hufanyi malipo kwa wakati, kampuni za umeme na gesi au mafuta zitakuchukulia hatua za kisheria kwa kupitia shirika linalodai na kukusanya malipo yasiyolipwa kwa wakati. Hatua hii itaonekana kwenye ripoti yako ya mkopo.

This facility is
smoke free.



Sheria katika nchi ya Marekani zimewekwa kuhifadhi haki zako. Kama mkazi wa Marekani, inabidi ujue haki zako za kisheria na majukumu yako.

Haki Zako

Kama mkimbizi, una haki sawa na mtu yeyote mwingine anayeishi Marekani. Haki hizi ni pamoja na uhuru wa kutoa maoni yako, uhuru wa dini, uhuru wa kuhudhuria mikutano. Huwezi kukamatwa au kuwekwa jela kwa kutoa maoni yako, kufuata dini yako, au kukutana na kikundi cha marafiki zako. Una uhuru wa kuabudu, kuvaa nguo unazotaka, kufanya shughuli zako za kila siku kama unavyopenda lakini lazima ufuate sheria za serikali ya Marekani na sheria za mahali unapokaa.

Wakazi wote wa Marekani wanastahiki kupata kwa usawa hifadhi ya haki zao kwenye mambo ya ajira, nyumba, elimu, na uwezo wa kupata huduma za serikali. Sheria ya Marekani hairuhusu ubaguzi kwa kuangalia asili ya mtu, dini yake, au nchi anayotoka. Ijapokuwa baadhi ya matukio ya hivi karibuni yamesababisha woga mkubwa, huzuni, na ghadhabu miongoni mwa Wamarekani, karibu Wamarekani wote hawawabagui wahamiaji au wakimbizi. Hii ni kwa sababu Wamarekani wengi wana mabibi na mababu ambao walikuwa wahamiaji au wakimbizi. Lakini kuna baadhi ya Wamarekani ambao wana mawazo yasiyo mazuri juu ya watu waliokuja Marekani kutoka nchi nyingine. Kama ukibaguliwa au ukinyimwa haki zako kwa sababu ya namna unavyoonekana au kwa sababu ya lugha unayozungumza, una haki ya kupata hifadhi ya polisi na kuchukua hatua ya kisheria. Huduma za msaada wa sheria zinapatikana katika jamii nyingi. Shirika la makazi mapya linaweza kukusaidia kupata maelezo ya huduma hizi.

Kama ukituhumiwa na kosa la jinai Marekani, unaendelea kuzingatiwa kuwa mtu asiye na hatia mpaka itakapothibitishwa kuwa una hatia. Una haki ya kupata wakili ambaye atakuwakilisha mahakamani. Kama huwezi kumiliki kuwa na



wakili, mahakama itamlipa wakili akuwakilishe. Lakini kama ukivunja sheria, shirika lako la makazi mapya haliwezi kuingilia kwa niaba yako.

Majukumu Yako

Kuna aina tatu za sheria Marekani. Sheria za serikali ya Marekani, kama vile sheria dhidi ya uuzaji wa dawa za kulevya ambazo zinamhusu kila mtu anayeishi Marekani. Sheria za majimbo zinatofautiana kutoka jimbo moja hadi jimbo jingine; kwa mfano, kwenye baadhi ya majimbo unaweza kupata leseni ya kuendesha motokaa ukiwa na umri wa miaka 16, wakati kwenye majimbo mengine ni lazima uwe na umri wa miaka 18. Sheria za mahali unapokaa ni sheria zinazotumika kwenye mji fulani au mkoa fulani. Inakubidi uelewe sheria za Marekani kwa sababu nyingi za sheria hizi zinatofautiana na sheria katika nchi yako unayotoka.

Marekani, unaweza kupewa adabu ukivunja sheria, hata ikiwa huijui hiyo sheria uliyoivunja. Kama mkimbizi, unahitaji kukumbuka kwamba hukumu ya baadhi ya makosa ni kurejeshwa nchi uliyotoka. Uliza shirika lako la makazi mapya kama una maswali kuhusu sheria hizi.



Yafuatayo ni mambo muhimu ambayo inabidi uyajue kuhusu sheria za Marekani:

- Ni kinyume cha sheria kununua, kuuza, au kutumia aina yoyote ya madawa ya kulevya. Ukivunja sheria hii, utarejeshwa nchini unakotoka. Inabidi uhakikishe kutoka shirika lako la makazi mapya kuhusu madawa ambayo nchini kwako yanaruhusiwa kisheria lakini Marekani hayaruhusiwi.
- Ni kinyume cha sheria kumtesa mtu kimwili (kumpiga) mke/mume wako au mtoto. Ni kinyume cha sheria pia kuwaacha watoto wako bila ya kuangaliwa. Kwenye baadhi ya nchi ni kawaida kwa watoto wakubwa kuangalia wadogo zao, lakini Marekani, watoto wadogo lazima waangaliwe na watu wazima. Kumpiga mtoto ni kumtesa mtoto, na kumwacha mtoto bila ya kusimamiwa kunaonekana kama kutomtunza mtoto. Makosa yote mawili yanaweza kusababisha watoto wako waondolewe nyumbani kwako na shirika la hifadhi ya watoto.

- Kumwingilia kimwili mtoto (mwenye umri chini ya miaka 18 karibu kwenye majimbo yote) ni kuvunja sheria. Kosa la kumwingilia mtoto mwenye umri huu kunaweza kusababisha uwekwe jela na kufukuzwa nchini. Ndoa ya zaidi ya mke/mume mmoja (polygamy) ni kuvunja sheria pia.
- Kama una watoto na ukapata talaka au wewe na mke/mume wako mkawa mnaishi mbali mbali kisheria, inabidi uendelee kuwapa watoto wako msaada wa kifedha kwa kumpa mke/mume wako wa zamani malipo ya kila mwezi. Msaada huu unaitwa msaada wa watoto na ni wajibu wa kisheria. Kutotoa msaada wa watoto kunaweza kuhatarisha hali yako ya uhamiaji.
- Watoto Marekani hawaruhusiwi kunywa pombe mpaka watakapofika umri wa miaka 21, na watoto hawaruhusiwi kununua pombe madukani. Kwa kawaida, ni kinyume cha sheria pia kunywa pombe nje au barabarani, isipokuwa kwenye sehemu zilizowekwa maalum kama kwenye baa au hoteli.
- Maneno ya kushambulia au matendo ya kumtesa mtu kijinsia kwenye mahali pa kazi ni kinyume cha sheria.
- Ni kinyume cha sheria kuwa na bunduki au bastola bila ya leseni. Kwenye sehemu nyingi, ni kinyume cha sheria kuwinda wanyama au kuvua samaki bila ya leseni, na ni lazima ujifunze na uzifuate sheria za mazingira.
- Ni kinyume cha sheria kuendesha motokaa kama huna leseni ya Marekani au kama umekunywa pombe. Kuendesha motokaa wakati umekunywa pombe zaidi ya kiwango kilichowekwa ni hatia na unaweza kunyanganywa leseni yako, kuwekwa jela, na labda kufukuzwa nchini.
- Majimbo mengi yana sheria kuhusu utumiaji wa mikanda ya viti kwenye motokaa. Wazazi wanatakiwa wawafunge watoto wao mikanda na watumie viti maalum vya usalama

kwa watoto wachanga. Kuna sheria za mikanda kwa watu wazima pia.

- Ni kinyume cha sheria kuvuta sigara kwenye maeneo ya umma kama majengo ya sinema na kwenye maofisi. Kwenye maeneo mengine kama hoteli kunaweza kuwa na sehemu maalum ya kuvuta sigireti. Kama unavuta sigireti, uliza shirika lako la makazi mapya kuhusu sheria hizi kwenye eneo lako.
- Marekani kuna sheria ambazo zinawahifadhi wanyama. Ni kinyume cha sheria kuwapiga wanyama, kutowatunza, kuwatesa, au kuwatoa mhanga.

Hali Yako ya Kisheria na Uraia Wako

Kufanya makazi mapya ni uamuzi wa kudumu kwa wakimbizi wengi. Kuruhusiwa kuingia Marekani kama mkimbizi kunakuruhusu kuishi Marekani daima na mwishowe kuomba kuwa raia.

Mwaka wako wa kwanza Marekani, utakuwa na hali ya kuwa mkimbizi. Wakati huu ni lazima uchukue nakala ya kadi yako ya I-94 na kadi ya EAD wakati wote kama ushahidi wa hali yako halali ya kuwa Marekani. Kama mkimbizi, unaweza kufanya mambo yafuatayo:

- Kusafiri popote nchini Marekani
- Kununua nyumba au ardhi
- Kuajiriwa
- Kuhudhuria shule
- Kumdhamini mke/mume wako au watoto wako ambao hawajaolewa na wana umri chini ya miaka 21 kama mmepoteana kwa sababu ya kukimbia kutoka nchi yenu

ya asili. Ukitaka mke/mume wako au watoto waje kukaa pamoja nawe Marekani, shirika lako la makazi mapya litakueleza mambo na taratibu zinazotakiwa.


Wakati una hali ya kuwa mkimbizi, huwezi kupata pasipoti ya kusafiria ya Marekani, kujiunga na jeshi, kupiga kura wakati wa uchaguzi, au kuajiriwa kwenye kazi za serikali zinazohitaji raia wa Marekani. Ijapokuwa unaweza kusafiri kokote nchini Marekani, ni lazima uiarifu USCIS ukihama. Unapobadilisha anuani una siku kumi za kuijulisha USCIS. Shirika lako la makazi mapya litakusaidia kujaza fomu inayotakiwa.

Wakati una hali ya kuwa mkimbizi, huwezi kusafiri nje ya Marekani bila ya ruhusa kutoka USCIS. Kama ni lazima usafiri nje ya Marekani, shirika lako la makazi mapya litakueleza vipi kupata ruhusa hiyo. Ukirejea nchi yako ya asili, huenda usiruhusiwe kuingia Marekani tena.

Wakimbizi wa kiume wenye umri baina ya miaka 18 na 25 lazima wajiandikishe na shirika la serikali linaloitwa “Selective Service”. Shirika hili linaweza kuita watu wajiunge jeshini, kwa kawaida wakati wa vita. Kwa wakati huu, wanajeshi wote wa jeshi la Marekani ni watu wanaojitolea. Watu wasiojiandikisha wanaweza kuwa na shida ya kupata hali ya ukazi wa kudumu na kupata uraia.

Baada ya mwaka 1 wa kuishi Marekani, unaweza kuomba kuwa mkazi wa kudumu. Wakazi wa kudumu wanaweza kusafiri nje ya nchi (hawawezi kukaa nje ya nchi kwa muda wa zaidi ya mwaka mmoja) na wanaweza kujiunga kwenye jeshi la Marekani, lakini hawawezi kupiga kura wakati wa uchaguzi wa Marekani au kuwa na kazi za serikali ya Marekani ambazo zinahitaji wafanyakazi walio raia. Shirika lako la makazi mapya litakueleza vipi unaweza kuwa mkazi wa kudumu.

Baada ya kukaa Marekani muda wa miaka 4 na miezi 9, unaweza kuomba kuwa raia. USCIS au shirika lako la makazi mapya linaweza kukueleza mambo yanayotakiwa kuwa raia. Miongoni mwa mambo haya ni kuwa na tabia nzuri na kuwa na ujuzi wa kimsingi wa lugha ya Kiingereza pamoja na historia na serikali ya Marekani. Watu waliopata uraia kwa kujiandikisha wana haki sawa na raia waliozaliwa Marekani.



Marekani ni nchi ya wahamiaji walioleta pamoja nao desturi na mila za utamaduni wao. Kwa hivyo hakuna utamaduni wa aina moja Marekani. Lakini Wamarekani wanakubaliana juu ya tabia nzuri zinazofaa, na wanataraji watu wengine wafuate tabia hizo. Tabia hizo huenda zikawa tofauti na zile za utamaduni wako, na huenda zikaonekana kuwa za kigeni au zikaenda kinyume na tabia zinazokubalika nchini kwako. Utaweza kufaulu Marekani ukijaribu kuzifuata tabia hizi na ikiwa uko tayari kufanya mabadiliko, na kuuliza maswali juu ya tabia ambazo huzielewi. Haya hapa ni mambo ambayo inabidi ujue kuhusu na tabia na mambo wanayothamini Wamarekani:

Tabia ya kuwa wachangamfu. Wamarekani wanapendelea hali ya tabia ya kuwa wachangamfu zaidi ya watu wengine wengi. Kwenye hali za kawaida, Wamarekani huitana kwa kutumia majina yao ya kwanza. Kwenye hali za kikazi, majina ya mwisho hutumiwa kabla ya mtu kutambulishwa rasmi, lakini wakuu wengi wa kazi na wafanyakazi wanapendelea kutumia majina yao ya kwanza. Cheo cha heshima kama “Daktari” hutumika kwenye hali zilizo rasmi tu. Wamarekani wanapenda kutabasamu sana, na hutabasamu wakiamkiana na marafiki na hata wakiamkiana na wageni.

Kufika kwa wakati bila ya kuchelewa. Kuangalia saa kunathaminiwa sana. Wamarekani wanajaribu kufika kwa wakati na wanataraji wengine kuweka wakati pia. Kufanya miadi na kuiweka miadi hiyo ni jambo la lazima kwenye hali iliyo rasmi na isiyo rasmi. Kama hufanyi miadi kabla ya kwenda kumwona mtu ofisini kwake kikazi huenda usimwone mtu huyo, na kama huwezi kwenda kwenye miadi uliyoweka au unataraji kuchelewa zaidi ya dakika 15, inabidi upige simu, ueleze kwamba utachelewa, na inabidi uombe msamaha.

Kuwa na faragha. Wamarekani wanathamini sana faragha yao. Si jambo la kawaida kwa watu kuwatembelea wengine majumbani mwao bila ya kupiga simu kwanza au kualikwa. Mambo ya fedha ni mambo ya mtu binafsi, na si tabia nzuri



kuuliza mtu anapata mshahara kiasi gani au alinunua nyumba au motokaa yake kwa bei gani. Pia ni tabia mbaya kumwuliza mtu usiyemjua au mtu ambaye umekutana naye hivi karibuni maswali binafsi.

Usafi wa mwili. Wamarekani wengi wanaoga kila siku, wanapiga mswaki na mara kwa mara wanaosha nywele zao kwa kutumia shampuu, na pia wanafua nguo zao sana. Maduka yanauza bidhaa nyingi zinazowasaidia watu kuepuka kuoenekana wachafu au kunuka majasho. Usafi wa mwili ni muhimu sana hasa wakati wa kutafuta kazi na kuendelea kuwa na kazi hiyo, wakati wa kufanya mahojiano ya kazi na wakati uko kazini. Waulize wafanyakazi wa shirika lako la makazi mapya maswali juu ya usafi wa mwili.

Utoaji wa Bahashishi. Ni kawaida kumpa mwandikiaji chakula bahashishi ya asilimia 15 au asilimia 20 ya fedha unazodaiwa kwa chakula hotelini, na ni kawaida kumpa dereva wa tekisi pia asilimia 15 au asilimia 20 ya malipo ya tekisi. Usimpe polisi au ofisa wa serikali pesa au bahashisi kama shukrani kwa msaada wao.

Pombe na uvutaji sigireti. Ijapokuwa watu wanakunywa pombe Marekani, kuna sheria nyingi za utumiaji na uuzaji wa pombe. Uamuzi wa kunywa pombe unachukuliwa kama



ni uamuzi binafsi, na hapa Marekani si tabia mbaya kukataa kama ukikaribishwa kunywa pombe. Wamarekani wengi hawavuti sigireti, na wanataraji watu wengine wasivute sigireti wanapowatembelea majumbani mwao.

Usalama wa binafsi. Ijapokuwa kuna jinai na ujambazi hapa Marekani, hali ya jinai ni tofauti katika sehemu mbali mbali za nchi. Popote pale unapoishi, ni lazima uchukue hadhari ya kufunga kwa kufuli nyumba yako na motokaa yako, na kutokuwa pamoja nawe fedha nyingi, na kujua mitaa gani inabidi uiepuke wakati wa usiku.

Vitambulisho binafsi. Kwa sababu Marekani ina watu wengi, Wamarekani wanatumia vitambulisho wanapofanya mawasiliano ya kiserikali na ya kikazi. Ni lazima uchukuwe wakati wote nakala ya kadi yako ya I-94 na kadi yako ya EAD, na pia jina, anuani, na nambari ya simu ya shirika lako la makazi mapya. Kama hujui Kiingereza, chukua nambari yako ya simu na anuani yako na simu ya mtu yeyote ambaye unakwenda kumtembelea.

Harakati za kujifunza kuhusu tabia za Wamarekani na mambo wanayothamini na kujaribu kufuata tabia hizi ni sehemu ya kujirekebisha kiutamaduni. Kufanya marekebisho haya haina



maana kwamba inabidi uache sehemu zote za utamaduni wako. Kwa kweli, wakimbizi wengi wanafikiri kwamba wamefanikiwa kujirekebisha wakiwa wamejifunza na kuingiza sehemu za utamaduni wa Marekani kwenye baadhi ya sehemu za utamaduni wao.

Kukabiliana na Mshtuko wa Utamaduni Mpya

Matatizo ya kuwa kwenye utamaduni mpya ni pamoja na kuwa na hisia ya kutojiweza na kuvunjika moyo kwenye nchi yenye lugha usiyoielewa na utamaduni usiyouelewa. Kuwa na mshtuko wa utamaduni ni jambo la kawaida; mtu yeyote anayekwenda kuishi kwenye nchi nyingine anaweza kupata matatizo haya.

Kama una mfidhaiko wa utamaduni mpya, huenda ukahisi mambo yafuatayo:

- kuvunjika moyo kama huwezi kufanya shughuli zako za kila siku kama kwenda dukani au kusafiri kwa kutumia usafiri wa umma;
- kuchoka wakati wa mchana na kutoweza kulala usiku;
- kuhamaki na kuwa katika hali ya kusumbuka
- kuwa na huzuni na
- kutopenda kula

Kuhamia kwenye nchi mpya na ya kigeni ni jambo la kufadhaisha na lenye shida kwa wakimbizi wengi. Kila mtu anapata shida hizi kwa namna tofauti, lakini kuna hisia ambazo unaweza kuzitambua kama kutokuwa na hamu ya kufanya chochote, kukosa hisia ya kujiamini, kukosa hisia ya kujielewa mwenyewe, na kuvunjika moyo. Kwa kawaida hisia hizi ni za muda na huondoka baada ya muda. Wageni wengi wanaokuja Marekani wamepata hisia hizi na baada ya muda wanapata nguvu zaidi na uwezo wa kuzishughulikia hisia hizo.

Baadhi ya wakati hali hii ya kufadhaika inaweza kusababisha matatizo ya kuendesha maisha ya kila siku, kutoelewana katika familia, na hata kubughudhi jamaa nyumbani. Ni muhimu kutambua mfadhaiko na shida unazohisi, na kutafuta huduma zinazoweza kukusaidia, na kujipatia ujuzi wa kuondoa shida hizo.

Njia za kuweza kukabiliana na matatizo ya utamaduni mpya zinatofautiana baina ya watu na tamaduni mbali mbali. Labda tayari unao ujuzi wa kuhimili matatizo hayo, kama kula vizuri, kufanya mazoezi, na kupata usingizi wa kutosha; kukutana na marafiki au kuhudhuria tafrija ya jamii au tafrija ya utamaduni; kuweka malengo binafsi; na kuwasiliana na huduma za kidini kama msikiti, kanisa, na hekalu la mahali unapokaa. Baadhi ya watu wanajihisi vizuri wanapofanya na kufurahia jambo wanalolipenda au kusikiliza muziki wanaoupenda. Njia moja inayotumiwa na karibu wageni wote ni kujiunga na vikundi maalum kama vyama vya kusaidiana vilivyoundwa na watu wanaotoka nchi fulani au watu wa asili fulani.

Uliza shirika lako la makazi mapya kuhusu mambo haya.

Kubadili Wajibu Katika Familia

Jambo moja linalosababisha mfadhaiko mkubwa wakati wa kufanya makazi mapya ni mabadiliko ya wajibu katika familia. Baba, mama, vijana, watoto wadogo, na wazee, wote wanatambua kwamba maisha katika Marekani yanaweza

kubadilisha uhusiano baina yao. Hili ni jambo la kawaida katika kufanya makazi mapya, lakini linaweza kusababisha matatizo mwanzoni.

Wakimbizi wote, wanaume na wanawake, wana matatizo ya kujirekebisha katika kuchukua wajibu tofauti wa wanaume na wanawake wa Marekani. Wamarekani wanaamini kwamba kuna usawa baina ya wanawake na wanaume na wanathamini uwezo wa kujitegemea na uwezo wa kuwa na uhuru kwa wote wanawake na wanaume. Katika familia nyingi, mume na mke, wote wawili wanafanya kazi, na wanashirikiana katika majukumu ya kulea watoto.

Katika baadhi ya familia, ikiwa wazazi wote wawili wanafanya kazi, mke anaweza kupata mshahara mkubwa zaidi kuliko mumewe. Katika familia nyingine, mke huenda akawa na kazi na mume akawa hana. Katika familia kama hii, mume anatarajiwa kutunza watoto wakati wanapokuwa nyumbani. Katika hali kama hizi, wakimbizi wa kiume huhisi wamepoteza wajibu wao ya uongozi katika familia. Wakimbizi wa kike wanaweza wakahisi kwamba wamepata nafasi ya kujiamini lakini pia wanaweza kuhisi vibaya.

Kuhamia sehemu mpya kunaweza kusababisha hali ngumu kwa vijana, hasa vijana baina ya miaka 13 na 20, kwa sababu ni lazima wajirekebishe na maisha katika utamaduni mpya na wakati huo huo wanatarajiwa kuendelea na maisha yao ya asili nyumbani na katika jamii zao. Na inabidi wafanye hivi wakati wana mabadiliko ya kiumri kutoka hali ya kuwa kijana kwenda utuuzimani.

Kwa sababu wanajifunza Kiingereza kwa haraka zaidi kuliko wazazi wao, vijana huenda wakaombwa wawe wakalimani wa wazazi wao na wachukue majukumu mengine mapya. Mara kwa mara ni lazima waende shule na pia wafanye kazi. Wazazi

wanaweza kuhisi kwamba hawana uwezo wa kuwasaidia watoto wao kwa sababu ya kutofahamu vizuri mfumo wa elimu ya Marekani. Na vijana kwa kawaida hawawezi kuwasiliana na wazazi wao juu ya mfidhaiko wanaoupata.

Kama mifadhaiko hiyo ikiwa mikubwa, baadhi ya vijana huanza kuwa na tabia mbaya, kama kutohudhuria shule, kujiunga na magengi, au kutumia madawa ya kulevya. Tabia hizi zinaweza kusababisha matatizo zaidi kwa sababu kufanya mambo hayo ni kinyume cha sheria. Kwa wasichana wasioolewa, tabia mbaya zinaweza kuwasababisha kupata mimba.

Kubadilisha dhima ni shida kwa jamaa walio wazee, ambao wanaweza kufikiri kwamba wamepoteza hali yao ya zamani ya kuwa watu wenye ujuzi na uzoefu katika familia. Marekani, masisitizo juu ya vijana na uwezo wao wa kufanya kazi unaweza kuwafanya wazee wahisi kama wanapuuzwa na wajihisi ni watu duni. Matatizo ya kujifunza lugha mpya na utamaduni mpya yanaweza kusababisha wazee wahisi kuwa wapekwe. Wazee wanaweza kujiona kwamba hawana cheo cha kuheshimiwa katika jamii.

Matatizo ya uchumi yanayowakabili wakimbizi wazee yanaweza kuwa mazito. Baadhi ya wakimbizi wazee ambao walitaraji kustaafu na kupata pensheni wanaweza wakajikuta kwamba wanahitaji kazi, hasa kama wana umri chini ya miaka 65. Wakimbizi wenye umri zaidi ya miaka 65 wanaweza wakagundua kwamba mafao ya wale waliostaafu hayalingani na matarajio yao, na mafao wanayopatiwa walemavu hayawezi kugharimia malipo ya daktari, na/au familia zao hawawezi kuwahudumia kama wanavyohudumiwa nchini mwao. Matatizo haya ya uchumi, pamoja na kupoteza cheo chao cha heshima

na hisia ya kuwa wapweke, kunaweza kusababisha hisia za unyonge na mambo mengine ya afya ya akili.

Kama wewe au mtu katika familia yako mnaishi hamwezi kukabiliana na mfadhaiko wa maisha mapya Marekani, tafuteni msaada haraka. Mambo yanayohusu wajibu mpya katika familia ni lazima yajadiliwe wazi wazi kwenye madarasa ya kujirekebisha kiutamaduni au pamoja na mhudumu wa kesi yako wa Marekani. Shirika lako la makazi mapya linaweza kutafuta huduma zitakazoweza kukusaidia upate ujuzi wa kukabiliana na shida hizi na kukupatia uwezo wa kukabiliana na hali za mifadhaiko nyumbani.


Kufanya makazi mapya katika nchi ya kigeni ni jambo linalochukua muda mrefu. Huenda ukahitaji miaka 2 mpaka 5 kujirekebisha kabisa kwenye jamii yako mpya. Jaribu kuwa mwangalifu na ujaribu kutohukumu watu na jiwekee malengo ya maisha yajayo. Kuwasiliana kwa uaminifu, kuwa mwenye subira, na kuwa na tabia ya kushirikiana na wale wanaojaribu kukusaidia kutakusaidia sana katika kujirekebisha kwako. Kutakusaidia pia kuelewa maadili ya Wamarekani, kama kujitegemea na kuwa na uhuru. Kugundua utamaduni mpya ni jambo gumu, lakini kunaweza kukutajirisha kiutamaduni na kukupa hisia ya kutoshelezeka.


“*Hisia zangu kuhusu nchi hii ni tofauti sasa kutokana na hisia nilizokuwa nazo nilipofika mara ya kwanza. Nilipokuwa Vietnam, nilifikiri kwamba kuja Marekani ni kama kwenda peponi. Hivyo ndivyo watu walivyoniambia. Sasa, sifikiri Marekani ni kama peponi. Marekani ni bora zaidi tu kuliko Vietnam.*”

“*Ijapokuwa tunaishi Marekani, bado tuna haki ya kukumbuka na kuhifadhi desturi zetu. Bado tunajifunza maisha na mila za Wamarekani. Tunafuata baadhi ya desturi hizi, lakini wakati huo huo ni lazima tujue kwamba ijapokuwa hatuna nchi yetu wenyewe, bado tunakumbuka, tunatambua, tunathamini utamaduni wetu. Karibuni nyote ambao mnataraji kuja hapa Marekani.*”

“*Huwezi kujifunza mambo yote ya maisha ya hapa kwa muda wa miezi miwili. Inachukua miaka na miaka.*”

“*Nimebadilika katika muda wa mwaka huu mmoja uliopita. Sibisi kutaka kurudi nyumbani sasa kama nilivyohisi mwanzoni na siogopi tena kukabiliana na vitu vipya. Nimejifunza vipi kupata kazi bora kwa kujifunza Kiingereza.*”





Marekani Bara